Sifa za Kiutendaji za kazi ya Ukaguzi wa Ndani Ngazi ya Serikali za Mitaa

Sikika

2021

Sifa za Kiutendaji za kazi ya Ukaguzi wa Ndani Ngazi ya Serikali za Mitaa

Kwa kushirikiana na
Mradi wa Usimamizi Bora wa Fedha za Umma

Unaotekelezwa na:

giz Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit (GIZ) GmbH

Kwa niaba ya:

german cooperation
DEUTSCHE ZUSAMMENARBEIT

Schweizerische Eidgenossenschaft
Confédération suisse
Confederazione Svizzera
Confederaziun svizra

Swiss Agency for Development and Cooperation SDC

Co-funded by the European Union

2021

> “Wakati ambapo maendeleo na ustaarabu yanakuja na mtazamo wa mtu mmoja kuaminiwa kiasi cha kukabidhiwa mali ya mwingine; kuna umuhimu pia wa kuangalia kwa dhati uaminifu wa mtu anayekabidhiwa mali hizo.”

Richard Brown (1968), Historia ya Uhasibu na Wahasibu.

ORODHA YA VIFUPISHO

AC	Kamati ya Ukaguzi
CAG	Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali
CIA	Mdhibiti na Mkaguzi wa Ndani
COSTECH	Tume ya Sayansi na Teknolojia
CPA	Mhasibu Aliyethibitishwa na Bodi ya Wakaguzi na Wahasibu Tanzania
ERM	Usimamizi wa Vihatarishi vya Biashara
GARI-ITS	Mapendekezo ya Serikali ya Utekelezaji wa Ukaguzi wa Mfumo wa Kufuatilia Taarifa
GFS	Takwimu za Fedha za Serikali
GIZ	Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Ujerumani
IA	Mkaguzi wa Ndani
IAG	Mkaguzi Mkuu wa Ndani
IAGD	Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani
ICT	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
IIA	Taasisi ya Wakaguzi wa Ndani
INTOSAI	Shirika la Kimataifa la Kusimamia Taasisi Kuu za Ukaguzi
IPPF	Mfumo wa Kimataifa wa Uzoefu wa Kitaaluma
ISA	Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi
LGA	Mamlaka ya Serikali za Mitaa
MDAs	Wizara, Idara na Wakala za Serikali
MTEF	Mfumo wa Matumizi wa Muda wa Kati
PEFA	Usimamizi na Uwajibikaji katika Matumizi ya Fedha za Umma
PO-RALG	Ofisi ya Rais– Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
PPRA	Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma
PSE	Taasisi ya Utumishi wa Umma
RS	Sekretarieti ya Mkoa
SAI	Taasisi ya Juu ya Ukaguzi
SDC	Shirika la Maendeleo la Uswisi

SHUKRANI

Utafiti huu wa Sifa za Kiutendaji za kazi ya Ukaguzi wa Ndani Ngazi ya Serikali za Mitaa umefanikiwa kutokana na ushiriki na mchango wa watu wengi.

Tunashukuru kwa mchango wa utaalamu na fedha tuliopata kutoka kwa Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Ujerumani (GIZ) kupitia Programu ya Usimamizi wa Fedha na Utawala Bora. Tunatoa shukrani za kipekee kwa Vanja Ćurčić, ambaye alisimamia utafiti, pamoja na Thereza Ngunangwa, aliyefanya uhakiki wa ubora wa hadidu za utafiti na kuandika ripoti.

Tunapenda pia kumshukuru Mshauri Gustav Mtenga kutoka Taasisi ya Ukaguzi wa Ndani Tanzania kwa kuhakiki ubora wa ukalimani wa dodoso. Tunatambua pia mchango wa Richard Magongo alioutoa wakati wa mafunzo ya watafiti na pia Revocatus Wambura aliyekusanya takwimu kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa. Tunamshukuru pia Lilian R. Kallaghe kwa kutafsiri ripoti hii kutoka lugha ya Kiingereza kwenda kwenye Kiswahili.

Kutoka Sikika, tunashukuru kwa mchango wa Florian Schweitzer, ambaye alisimamia maandalizi na utekelezaji wa utafiti, uchambuzi wa taarifa/data zilizokusanywa, na kuandaa ripoti hii. Tunatambua mchango wa Daniel Mugizi na Joshua Nkila katika ukusanyaji wa takwimu kutoka kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Tunamshukuru pia Alphonce Chuwa, aliyeratibu mchakato wa ukusanyaji takwimu kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa na pia kunakili na kutafsiri takwimu na kuziweka katika mfumo ambao ni rahisi kusomeka. Tunatambua pia mchango wa Alice Monyo, ambaye alisimamia ubora wakati wote wa mchakato wa utafiti na uandishi wa ripoti hii.

Tunasema *asanteni sana.*

Irenei Kiria,

Mkurugenzi Mtendaji- Sikika

MUHTASARI

Dira ya Maendeleo ya Tanzania ya 2025 inabainisha “utawala bora na utawala wa sheria” kama kichocheo muhimu cha kukuza na kufikia maendeleo.

Ili kupunguza makosa ya utunzaji wa kumbukumbu, matumizi mabaya au upotevu wa rasilimali, mfumo wa usimamizi wa fedha za umma unategemea umadhubuti wa mfumo wa ukaguzi wa ndani ambao unasaidia nchi kufikia malengo yake ya maendeleo.

Tangu mwaka 2018, Wizara ya Fedha na Mipango na wadau wengine nchini wamekuwa wakishirikiana na washirika wa maendeleo kuhusu “Mkakati wa Taifa wa Kuendeleza Mfumo wa Ukaguzi wa Ndani katika Sekta ya Umma ya Tanzania” ili kuhakikisha kuwa kazi ya ukaguzi wa ndani inaendana na Mfumo wa Kimataifa wa Uzoefu wa Kitaaluma 2017. Viwango hivi vya kimataifa vinatakiwa kubadilisha hali ya taasisi za wakaguzi wa ndani kutoka kuwa mbinu ya “ukaguzi kwa menejimenti” hadi kuwa “ukaguzi wa menejimenti”. Mabadiliko mapya kama hayo ya kimkakati ni changamoto na yanaweza kuathiri uhusiano uliopo wa kimamlaka katika ngazi ya serikali za mitaa. Viwango hivyo pia vinapaswa kutumika katika ugatuaji na usimamizi wa fedha za umma nchini.

Utafiti huu unalenga kuchangia katika mjadala wa mchakato wa mageuzi kwa kulinganisha maoni ya wadau kuhusu utendaji na sifa za kazi ya ukaguzi wa ndani katika ngazi ya serikali za mitaa na viwango vya kimataifa, na kutoa mapendekezo kwa watunga sera kuhusu jinsi kazi ya ukaguzi wa ndani inavyoweza kurekebishwa ili iendane na viwango vya kimataifa.

Mbinu iliyotumika

Utafiti huu unafuataMfumo wa Kimataifa na Uzoefu wa Kitaaluma kwamba utendaji na sifa za kazi ya ukaguzi wa ndani zinahusiana. Viwango vilivyochaguliwa vya utendaji na sifa vilifanyiwa upembuzi yakinifu katika maeneo mbalimbali kwa kujumuisha vitengo vya ukaguzi wa ndani, kamati za ukaguzi na kamati za fedha kutoka kwa Mamlaka sita za Serikali za Mitaa. Mamlaka zilizochaguliwa kuunda sampuli ya uwiano wa kijiografia zilijumuisha: Arusha, Babati, Dodoma, Mbeya, Mwanza na Korogwe.

Katika ngazi ya Serikali kuu, utafiti huo ulihusisha Kitengo cha Mkaguzi Mkuu wa Ndani pekee kwani Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa hazikujibu maombi ya usaili kwa wakati. Majibu ya wahojiwa wote wa kundi lengwa yalilinganishwa ili kuona ni wapi wadau mbalimbali wa kazi ya ukaguzi wa ndani wanakubali au hawakubaliani kuhusu masuala ya utendaji, masuala ya sifa na mapendekezo.

Matokeo

TShughuli ya ukaguzi wa ndani huongeza thamani katika mfumo wa usimamizi wa fedha za umma nchini kwa vile unazingatia malengo ya kitaasisi na matarajio ya usimamizi. Pia zinatoa huduma za ushauri kwa lengo la kuimarisha utawala, kudhibiti athari na udhibiti kwa wadau katika ngazi ya serikali za mitaa na serikali kuu. Hata hivyo, thamani zaidi inaweza kuongezwa kwa kuzingatia mazingira ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, kama vile hali duni ya ufadhili au ukiukwaji wa kanuni, ambavyo vinaweza kuwa sababu kuu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kutozingatia udhibiti wa ndani.

Mipango ya ukaguzi wa ndani inategemea tathmini ya vihatarishi iliyoandikwa, lakini uhaba wa rasilimali, udhaifu katika kuratibu na ushirikiano katika kazi ya ukaguzi wa nje huzuia ushughulikiaji bora wa ukaguzi na kusababisha kujirudia rudia kwa juhudi zilizofanyika.

Shughuli za ukaguzi hutegemea uhakiki wa ubora wa ndani na nje, na wakaguzi wa ndani hupewa ushauri na msaada ili waweze kuendana na viwango vya kimataifa. Lakini, shughuli za dharura na programu za maendeleo ya wafanyakazi zinakwamisha Mamlaka za Serikali za Mitaa kutokana na uhaba wa rasilimali zilizopo.

Kukosekana kwa mawasiliano kwa wakati kati ya wakaguzi wa ndani katika ngazi ya serikali za mitaa na mamlaka za serikali kuu, kunasababisha kutozingatiwa kwa ripoti ya ukaguzi. Aidha, uwepo wa menejimenti wakati wa vikao vya Baraza la Madiwani na kamati ya fedha ya halmashauri kunaweza kuwakatisha tamaa wakaguzi wa ndani. Katika hali hiyo, si rahisi kwa wakaguzi hao kutoa taarifa za mapungufu makubwa yanayotilia shaka uadilifu au umahiri wa menejimenti husika.

Kuna utaratibu rasmi wa ufuatiliaji wa mapendekezo ya ukaguzi, lakini majibu mepesi au yasiyoeleweka ya menejimenti yanaweza kukwamisha udhibiti wa vihatarishi ambavyo havikubaliki kwa taasisi.

Hitimisho

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa upeo wa kazi ya ukaguzi wa ndani ni mpana, lakini unakwamishwa na uhaba wa rasilimali: fedha na idadi ya wakaguzi wa ndani haitoshi kukamilisha kwa wakati shughuli zilizopangwa na zile za dharura. Changamoto nyingine ni kukosekana kwa uhuru wa wakaguzi wa ndani: wakaguzi wa ndani wanaripoti kiutendaji kwa kamati ya ukaguzi ambayo inaundwa na wasimamizi wakuu wanaomshauri mtendaji mkuu (Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri), ambaye anawawakilisha wakaguliwa. Hii inamaanisha kwamba mfumo bado unafuata mbinu ya zamani ya "ukaguzi kwa menejimenti".

Mapendekezo

Mapendekezo yafuatayo yanaweza kuchangia katika mjadala wa kina na wa muda mrefu kwenye mchakato wa kuleta mabadiliko ya maendeleo katika mfumo wa ukaguzi wa ndani, ili kuendana na viwango vya kimataifa vya ukaguzi wa ndani..

Kuongeza thamani kwa kuboresha uratibu kati ya mamlaka za serikali za mitaa na serikali kuu.

- Kazi ya ukaguzi wa ndani haina wafanyakazi wa kutosha, ujuzi au utaalamu katika maeneo mbalimbali yenye viashiria hatarishi. Ni vyema kujadili jinsi ya kutafuta wataalam wengine wa kufanya shughuli za ukaguzi wa ndani na kutafuta fedha za kufadhili shughuli hizo kwa kuzingatia kwamba vyanzo vya mapato vya Mamlaka za Serikali za Mitaa ni vichache.
- Afisa Mratibu wa Viashiria Hatarishi wa Mamlaka ya Serikali ya Mitaa anapaswa kushauri iwapo mchango wa serikali kuu katika mchakato wa kuandaa mipango pia ni kipaumbele cha Mamlaka ya Serikali ya Mitaa, kulingana na tathmini ya vihatarishi iliyofanywa.
- Wakaguzi wa ndani wanahitaji mafunzo zaidi juu ya kufanya uchambuzi wa vyanzo vya msingi vya vihatarishi. Ikiwa chanzo cha msingi ni mtendaji katika ngazi ya serikali kuu, mkaguzi wa ndani anapaswa kuainisha wanaowajibika kwenye utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi, kupitia Kitengo cha Mkaguzi Mkuu wa Ndani.

Kuimarisha mchakato wa kupanga ili kuhakikisha kuwa mipango ya ukaguzi wa ndani ina nyenzo za kutosha na inaratibiwa na Ofisi ya ukaguzi wa nje.

- Kitengo cha udhibiti wa athari kipewe fedha za kutosha na mafunzo ya kina zaidi.
- Wakaguzi wa ndani na chombo cha uangalizi cha Mamlaka ya Serikali za Mitaa wanapaswa kuhakikisha kuwa mpango kazi wa ukaguzi wa ndani unalingana na rasilimali zilizopo.
- Kiutendaji, Wakaguzi wa ndani wanapaswa kuripoti kwa chombo cha uangalizi cha Mamlaka ya Serikali ya Mitaa ili kuhakikisha uhuru wake wa kitaasisi na kujenga uaminifu kwa shughuli ya ukaguzi wa nje.

Kuimarisha mchakato wa ushiriki wa ukaguzi ili kushughulikia kazi za dharura na kuhakikisha umahiri na utendaji wa wakaguzi wa ndani.

- Mfumo wa Kimataifa wa Uzoefu wa Kitaaluma unapaswa kuwa sehemu ya mtaala wa wahasibu. Wakaguzi wa ndani wanatakiwa kuendelea kupata mafunzo kuhusu mabadiliko yanayoendelea ya Mfumo wa Kimataifa wa Uzoefu wa Kitaaluma.
- Mipango na bajeti za ukaguzi wa ndani inapaswa kujiandaa kwa mambo 'yasiyotarajiwa' na kutoa posho ili kushughulikia dharura zinapojitokeza.
- Wakaguzi wa ndani wanapaswa kuwasilisha matokeo ya programu ya uhakiki wa ubora na maboresho kwa kamati ya fedha. Kamati inaweza kuleta mahitaji ya rasilimali kwa baraza la madiwani wakati bajeti ya mwaka ya Mamlaka ya Serikali ya Mitaa inajadiliwa na kupitishwa.
- Inawezekana pia kujadili uwezekano wa kuandaa mfumo shirikishi wa kupanga, kufuatilia na kutathmini mipango ya maendeleo ya wafanyakazi katika ngazi ya serikali ya mitaa na serikali kuu.

Lengo ni kuimarisha uratibu wao na kuhakikisha kuwa ujuzi na utaalamu wa kada ya ukaguzi wa ndani unalingana na maeneo yenye viashiria hatarishi yaliyopewa kipaumbele.

Kuimarisha mchakato wa kuripoti ili kuhakikisha matokeo ya ukaguzi yanazingatiwa wakati wa shughuli ya usimamizi.

- Kitengo cha Mkaguzi Mkuu wa Ndani na mamlaka nyingine za serikali kuu ziwe na ratiba ya mawasiliano ili kusaidia kuratibu majibu ya mapendekezo ya ukaguzi kutoka ngazi ya serikali za mitaa.
- Wakaguzi wa ndani watoe taarifa kwa kamati ya fedha ya baraza la madiwani, ambayo ina jukumu la kudhibiti na kusimamia fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa.
- Wakaguzi wa ndani wanapaswa kuwa na mamlaka ya kuwasilisha ripoti ya ukaguzi wa ndani kwa kamati ya fedha ikiwa majibu ya menejimenti yatachelewa kutolewa bila sababu/uhalalisho.
- Wakaguzi wa ndani wanapaswa kukutana na kamati ya fedha bila menejimenti kuwepo ili kuhakikisha kuna uhuru na kwamba malengo ya mkaguzi wa ndani yanafikiwa.
- Wakaguzi wa ndani wanapaswa kupokea mwongozo kuhusu mahitaji ya kisheria ili kutoa taarifa pale wanapohisi udanganyifu au kutofuatwa kwa sheria na kanuni.
- Kujadili jinsi wajumbe wa kamati ya fedha wanavyoweza kupatiwa taarifa na mafunzo zaidi ili waelewe masuala ya ukaguzi na jinsi yanavyoathiri wajibu wao wa kudhibiti na kusimamia fedha za Mamlaka ya Serikali ya Mitaa.

Kumarisha mchakato wa ufuatiliaji ili kuhakikisha kuwa viashiria hatarishi vinapunguzwa hadi kiwango kinachokubalika.

- Ripoti za ukaguzi wa ndani zinapaswa kuchanganua mapendekezo ya viashiria hatarishi ambayo yaliripotiwa kama yametekelezwa, yalitekelezwa kwa kiasi, au hayakutekelezwa kabisa.
- Chombo cha usimamizi cha Mamlaka ya Serikali ya Mtaa kinapaswa kulinganisha mapendekezo ya viashiria hatarishi yaliyotekelezwa kwa kiasi au ambayo hayajatekelezwa na maelezo ya menejimenti yenye mantiki ili kutathmini kama athari zilizojitokeza zinakubalika kwa taasisi. Chombo cha uangalizi kinapaswa kuchukua hatua zinazofaa za kiutawala au kinidhamu dhidi ya watu binafsi au taasisi.
- Inapaswa kujadili ikiwa Kitengo cha Mkaguzi Mkuu wa Ndani kinaweza kufanya uchambuzi wa kimfumo na wa kina wa gharama na faida ya mapendekezo ya ukaguzi.

Yaliyomo

Orodha ya Vifupisho.....i

Shukrani.....ii

Muhtasari.....iii

1 Utangulizi.....1

1.1 Ukaguziwa Ndani.....1

1.2 Kazi ya Ukaguzi wa Ndani katika Ngazi ya Serikali za Mitaa.....1

1.3 Kufanya Marekebisho kwa Kazi ya Ukaguzi wa Ndani.....3

1.4 Malengo ya Utafiti.....5

1.5 Muundo wa Ripoti.....5

2 Mbinu za Utafiti.....6

2.1 Maandalizi.....6

2.2 Kazi za Nje.....7

2.3 Uchambuzi.....7

2.4 Vikwazo.....9

3 Matokeo.....9

3.1 Kuongeza Thamani.....9

3.2 Mipango.....11

3.3 Kushiriki katika Ukaguzi.....12

3.4 Utoaji Taarifa.....14

3.5 Ufuatiliaji.....16

4 Mjadala.....18

4.1 Ongezeko la Thamani.....18

4.2 Kupanga.....19

4.3 Ushiriki katika Ukaguzi.....20

4.4 Utoaji Taarifa.....21

4.5 Ufuatiliaji.....22

5 Hitimisho.....24

6 Mapendekezo.....25

Orodha ya Marejeo.....27

1 Utangulizi

1.1 Ukaguzi wa Ndani

Mahitaji ya ukaguzi yanatokana na hitaji la taasisi la kuwa na njia huru za uhakiki ili kupunguza makosa katika uhifadhi wa kumbukumbu, matumizi mabaya ya mali au upotevu wa rasilimali. Awali, wakaguzi wa ndani walikuwa na majukumu ya kawaida ndani ya taasisi na mara nyingi walisaidia wakaguzi wa nje katika kukagua miamala ya kifedha au shughuli zingine zinazohusiana na uhasibu. Lakini ugatuaji wa madaraka na umbali kati ya wasimamizi na watoa maamuzi yalipelekea tasisi kubadilisha miundo, kuboresha udhibiti wa athari, na kuanzisha safu za udhibiti. Maendeleo hayo pia yalibadilisha hali ya taasisi za wakaguzi wa ndani kutoka kwenye mfumo unaosisitiza "ukaguzi kwa menejimenti" kwenda kwenye "ukaguzi wa menejimenti"[1].

Kwa sasa, Taasisi ya Wakaguzi wa Ndani inaelezea ukaguzi wa ndani kama shughuli huru, yenye lengo la kuhakiki na kushauri ili kuongeza thamani na kuboresha shughuli za taasisi husika. Husaidia taasisi kutimiza malengo yake kwa kuleta mifumo ya kinidhamu ya kutathmini na kuboresha ufanisi na udhibiti wa vihatarishi, na udhibiti wa michakato ya utawala[2]. Kuanzishwa kwa michakato ya utawala bora, kama vile kugawana majukumu na wajibu kwa uwazi, ni muhimu ili kuhakikisha kwamba maslahi na maamuzi ya mtu binafsi yanawiana na malengo ya taasisi. Usimamizi wa vihatarishi ni mchakato muhimu wa kutambua matukio yanayoweza kuathiri vibaya malengo ya taasisi, kama vile matumizi mabaya ya fedha au rasilimali watu, ukiukaji wa sheria na kanuni, au taarifa potofu zinazoleta kutoaminika kwa ripoti ya kifedha ya taasisi. Ili kupunguza dosari hizo zibaki kuwa katika kiwango kinachokubalika, taasisi huweka udhibiti mbalimbali wa ndani, kama vile mifumo ya usimamizi wa mali, mifumo ya manunuzi, mifumo ya usimamizi wa rasilimali watu, mifumo ya uhasibu na mifumo mingine ya udhibiti.

Majukumu na wajibu wa wakaguzi wa ndani na wakaguzi wa nje yanaendana na wakati mwingine yanakuwa sawa, lakini kuna tofauti maalum ambazo mara nyingi hazipewi uzito stahiki au hata wakati mwingine huchanganywa. Wakaguzi wa ndani wameajiriwa na taasisi, lakini wanatakiwa kuwa huru kutokana na shughuli wanazokagua ili kuepusha mgongano wa kimaslahi. Ili kuhakikisha uhuru wa wakaguzi wa ndani, wanapaswa kuwa na uwezo wa kuwafikia moja kwa moja tena bila vikwazo wale wote wanaohusika na usimamizi wa taasisi. Wakaguzi wa ndani lazima wafuate Mfumo wa Kimataifa wa Uzoefu wa Kitaalamu (IPPF) uliotangazwa na Taasisi ya Wakaguzi wa Ndani. Kwa upande mwingine, wakaguzi wa nje hawana maslahi kwa sababu hawajaajiriwa na taasisi inayokaguliwa. Wao hufanya kazi mara moja kwa mwaka na, kwa hivyo, hawana uwezo wa kutoa ushauri wa kina wa jinsi ambavyo mambo yanahitaji kubadilika. Wakaguzi wa nje lazima wafuate Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA) vinavyotolewa na Shirikisho la Kimataifa la Wahasibu. Licha ya tofauti hizo, wakaguzi wa ndani na nje wanapaswa kuratibu kazi zao ili kuhakikisha ukaguzi wa kina unafanyika na kuepuka kurudia rudia kazi. Wanaweza pia kupeana idhini ya kupata au kuifikia mipango na ripoti za ukaguzi na kufanya mikutano ya mara kwa mara ili kujadili mambo yenye maslahi kwa pande zote mbili. Muhimu zaidi, mkaguzi wa nje ana wajibu wa kutathmini ufanisi na umakini wa shughuli za ukaguzi wa ndani na ufuasi wake wa viwango vya kitaaluma.

1.2 Kazi ya Ukaguzi wa Ndani katika Ngazi ya Serikali za Mitaa

Wakaguzi wa ndani wameajiriwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) na huunda kitengo tofauti cha huduma katika muundo wa taasisi yao. Wana wajibu wa "kutathmini ubora na matumizi ya uhasibu, udhibiti wa fedha na uendeshaji", ufuatiliaji wa majibu ya menejimenti kwa ripoti za ukaguzi wa ndani na kusaidia menejimenti katika utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa ndani na nje. [3] Wakaguzi wa ndani wanaripoti katika ngazi mbili: i) kuwezesha shughuli za kila siku za kazi za ukaguzi wa ndani, wanaripoti kiutawala (moja kwa moja) kwa mtendaji wa mkuu wa halmashauri, ambaye ni mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri; na ii) pia wanaripoti kiutendaji (sio moja kwa moja) kwa kamati ya ukaguzi na kwa Mkaguzi Mkuu wa Ndani. [4]

1 Sridhar Ramamoorti (2003), Chapter 1 Internal Auditing: History, Evolution, and Prospects, The Institute of internal Auditors Research Foundation, p. 4f.

2 Institute of Internal Auditors (2017), International Standards for the Professional Practices of Internal Auditing (Standards), p. 23.

3 Kanuni za Fedha za Umma (2004), Sehemu ya 34.

4 Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa , Wilaya ya Korogwe, Mkataba wa Huduma za Ukaguzi wa Ndani, Uk. 7.

Kamati ya ukaguzi inaundwa na angalau wakuu wawili (wa ndani) wa idara (ambao huteuliwa na mtendaji mkuu wa halmashauri) na wajumbe wawili (wa nje) kutoka nje ya baraza la madiwani. Kamati ya ukaguzi ina jukumu la kuidhinisha mpango mkakati wa ukaguzi wa ndani na mpango kazi wa mwaka, kupitia ripoti za ukaguzi wa ndani na nje, na kumshauri mtendaji mkuu wa halmashauri juu ya hatua za kuchukua. Kamati ya ukaguzi pia inaratibu mipango kazi ya ukaguzi wa ndani na ile ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. [5]

Kamati ya fedha ni kamati ya kudumu ya baraza la madiwani, ambayo inawajibika kwa maamuzi yote ya Halmashauri, ikiwa ni pamoja na usimamizi wa utendaji. Kamati ya fedha ina jukumu la kudhibiti na kusimamia fedha za Halmashauri.[6] Kupitia shughuli hiyo, inaweka mfumo wa udhibiti wa ndani kupitia miongozo ya kimaandishi ambayo mkurugenzi mtendaji lazima aigawe kwa maafisa wote wenye dhamana. Baada ya tathmini ya udhibiti wa ndani, mkaguzi wa ndani huwasilisha ripoti ya ukaguzi wa ndani kwa mkurugenzi mtendaji ambaye anaipeleka kwa kamati ya fedha. [7]

Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani (IAG) iliyopo ndani ya Wizara ya Fedha na Mipango ina jukumu la kuandaa sera na miongozo ya ukaguzi wa ndani pamoja na kufuatilia uzingatiaji wa sheria na kanuni. Idara ya IAG ina Sehemu ya Ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ambayo inajenga uwezo kwa kada ya mkaguzi wa ndani wa Halmashauri na kamati za ukaguzi. Idara ya IAG pia inakusanya ripoti za ukaguzi ili kuandaa muhtasari wa ripoti ya uchunguzi na kutoa mapendekezo makuu ya ukaguzi na kufuatilia hatua za kurekebisha. [8]

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ina jukumu la kufanya ukaguzi wa nje kwa taasisi zote za serikali zikiwemo Halmashauri. CAG hupokea ripoti za ukaguzi wa ndani kwa ajili ya uratibu na kupata ushirikiano mzuri wa wakaguzi wa ndani wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kama taasisi kuu ya ukaguzi nchini, CAG pia anawajibika kufanya tathmini ya nje, kwa kazi ya ukaguzi wa ndani.

Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) inatoa rasilimali, maagizo, na kujenga uwezo kwa wakaguzi wa ndani[9] na pia ina jukumu la kusimamia utendaji wa Halmashauri. Kwa hiyo, Kitengo cha Ukaguzi na Ufuatiliaji wa Fedha hufanya ukaguzi wa mara kwa mara na ufuatiliaji wa fedha zinazotumwa kwa Halmashauri na kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali[10]. Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) huteua wakurugenzi watendaji wa Halmashauri[11] na hivyo basi, ina uwezo wa kuzuia majibu yasiyojitosheleza kutokana na mapendekezo ya ukaguzi wa ndani na nje.

5 Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa (2009), Sehemu ya 12.

6 Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa (2009), Sehemu ya 5 na 6.

7 Memoranda ya Fedha za Serkali za Mitaa (2009), Sehemu ya 11 na 14.

8 Sheria ya Fedha za Umma (2010), Sehemu ya 38.

9 Wizara ya Fedha na Mipango na Programu ya Utawala Bora wa Fedha (2019), Mkakati wa Kuendeleza Mfumo wa Ukaguzi wa Ndani katika Sekta ya Umma Tanzania, Uk. 4.

10 Angalizo: Wakurugenzi watendaji wote wa halmashauri za miji wanateuliwa na Rais.

11 Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Ujerumani (2014), Sekretarieti ya Mkoa (Backstopping) – Ufuatiliaji na na Tathmini ya Udhibiti wa Ndani, Kitabu cha Washiriki, Uk. 17.

1.3 Kufanya Marekebisho kwa Kazi ya Ukaguzi wa Ndani

Dira ya Maendeleo ya Tanzania ya 2025 inabainisha "utawala bora na utawala wa sheria" kama kichocheo kikuu cha kukuza na kufikia maendeleo. "Utawala bora lazima ukuzwe kwa kukuza utamaduni wa uwajibikaji na kwa kubainisha wazi jinsi motisha unavyotolewa na kulingana na utendaji na jinsi zuio au vikwazo vinavyowekwa."[12] Katika kutekeleza dira ya maendeleo, Mpango wa tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26) unasisitiza umuhimu wa mfumo unaofanya kazi wa ufuatiliaji na tathmini unaotumia hatua zilizopo za udhibiti wa fedha na taarifa za ukaguzi wa ndani kutoka Wizara, Idara na Wakala wa Serikali za Mitaa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekretarieti ya Mkoa, kutathmini matumizi sahihi ya rasilimali fedha[13]. Mpango wa Maboresho wa Usimamizi wa Fedha za Umma V (2017/18 – 2021/22) pia unaeleza uimarishaji wa udhibiti wa ndani na kazi ya ukaguzi wa ndani kama changamoto kuu katika kuleta mageuzi. [14]

Tathmini ya Kitaifa ya Matumizi ya Umma na Uwajibikaji wa Fedha (PEFA) (2016) ilibaini changamoto mbalimbali za kimfumo na kimuundo kwa kazi ya ukaguzi wa ndani katika ngazi ya serikali za mitaa, kama vile hati za ukaguzi wa ndani ambazo hazijapangiliwa kulingana na mazingira ya halmashauri; mapungufu ya rasilimali watu, fedha na mazingira halisi; na kamati zisizo na tija za ukaguzi ambazo zinalenga kuidhinisha maamuzi badala ya kuchunguza na kuishauri menejimenti ya halmashauri.[15] Maoni haya pia yalithibitishwa na ripoti na tafiti nyinginezo kama vile Tathmini ya PEFA 2017, Ripoti Kuu ya Mwaka ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (2019), na uchambuzi uliofanywa na washirika wa maendeleo, kama vile Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japani na Programu ya Utawala Bora na Fedha. Ili kupunguza makosa katika kuhifadhi kumbukumbu, matumizi mabaya au upotevu wa rasilimali, mfumo wa usimamizi wa fedha za umma unategemea kazi thabiti ya ukaguzi wa ndani ambayo husaidia nchi kufikia malengo yake ya maendeleo.

1.3.1 Mfumo wa Kimataifa wa Uzoefu wa Kitaaluma (IPPF)

Katika miongo ya hivi karibuni, kumekuwepo na maendeleo makubwa kuelekea kufikia mwafaka wa kimataifa kuhusu viwango vya ukaguzi wa ndani ambavyo serikali zinapaswa kutimiza. Viwango vya kina zaidi vya Kimataifa vya Uzoefu wa Kitaaluma vilivyoandikwa na kutangazwa na Taasisi ya Wakaguzi wa Ndani (IIA). Viwango hivi na Kanuni za Maadili ni vipengele muhimu vya Mfumo wa Kimataifa wa Uzoefu wa Kitaaluma. Viwango vinajumuisha vigezo vikuu viwili:

- Viwango vya Sifa vinavyoshughulikia sifa za taasisi na watu binafsi wanaofanya ukaguzi wa ndani.
- Viwango vya Utendaji ambavyo vinaelezea asili ya ukaguzi wa ndani na kutoa vigezo vya ubora ambapo utendaji kazi wa huduma zitolewazo unaweza kupimwa.

Mwaka 2017, Bodi ya Kitaifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu iliidhinisha ubadilishwaji wa Mfumo wa Kimataifa wa Uzoefu wa Kitaaluma (IPPF) 2011 na kuweka lazima kwa wakaguzi wote wa ndani nchini Tanzania kutuma maombi na kuridhia matumizi ya IPPF 2017.

1.3.2 Mkakati wa Kuendeleza Mfumo wa Ukaguzi wa Ndani

Tangu mwaka 2018, Kitengo cha Mkaguzi Mkuu wa Ndani cha Wizara na Fedha na Mipango na wadau wengine nchini wamekuwa wakishirikiana na washirika wa maendeleo[16] juu ya Mkakati wa Kitaifa wa Kuendeleza Mfumo wa Ukaguzi wa Ndani katika Sekta ya Umma Tanzania (unaojulikana kama Mkakati).

Hatua ya kwanza ya mchakato huo ilijumuisha 'kufanya mahesabu na tathmini' ya mfumo wa kisheria, nyaraka za sera, na nyaraka za kiufundi ili kutoa muhtasari wa kile ambacho kimefanyika hadi kufikia sasa. Wakati wa tathmini hii, 'masuala yanayojirudia mara kwa mara' yaliainishwa. Katika hatua ya pili, warsha ya wadau ya mashauriano ilifanyika ili kutekeleza 'uchambuzi wa kutafuta chanzo' ili kuelewa na kushughulikia 'masuala yanayojirudia mara kwa mara'. Katika hatua ya tatu, vikundi kazi vya kitaalamu viliundwa ili kujadili suala hilo na kuandaa mwelekeo kwa kila 'suala linalojirudia mara kwa mara', ili kufikia malengo ya shughuli mbalimbali, kama vile kupitia upya mfumo wa kisheria wa kazi ya ukaguzi wa ndani, kurekebisha michakato na taratibu za kiutawala, na kuendesha warsha za kujenga uwezo na uhamasishaji kwa wadau husika kwa ajili ya utekelezaji.

12 Tume ya Mipango, (haina tarehe), Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025, Sehemu ya 4.3.

13 Wizara ya Fedha na Mipango (2021), Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26, Uk. 150.

14 Wizara ya Fedha na Mipango (2017), Mpango wa Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma V, Uk. 7.

15 PriceWaterhouseCoopers (2016), Consolidated Sub-national Government PEFA Assessment report, p. 82ff.

16 Programu ya Utawala Bora wa Fedha inafadhiliwa na Umoja wa Ulaya, Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Ujerumani (GIZ), na Shirika la Maendeleo la Uswisi (SDC).

Jedwali 1: Jedwali la Matokeo ya Mkakati wa Uendelezaji wa Mfumo wa Ukaguzi wa Ndani.

	Masuala yanayojirudia	Chanzo	Malengo
1	Utaratibu wa utoaji huduma bila motisha	Ushirikishwaji duni wa wakaguzi wa ndani (IAs) wakati wa kuandaa mpango wa kiutendaji	1. Ukaguzi wa ndani unahusisha kada mbalimbali. 2. Mpango uliopo wa kiutendaji kwa wakaguzi wa ndani unaendana na mahitaji ya IPPF 3. Vivutio vilivyoboreshwa kwa IAs wanaofanya kazi katika taasisi/ mashirika ya umma (PSEs) vipo.
2	Utendaji duni na kukosa uhuru wa kamati za ukaguzi (ACs).	Mapungufu ya kisheria Uelewa mdogo wa majukumu ya kamati (AC) Mapungufu katika muundo wa kuripoti wa kamati (AC) Rasilimali fedha zisizotosheleza.	1. Kamati za ukaguzi na uangalizi zimeanzishwa katika PSEs. 2. Kamati za ukaguzi katika PSEs zote ni huru na zinafanya kazi. 3. Uwajibikaji wa kamati ya ukaguzi unatekelezwa katika PSEs zote.
3	Udhibiti hafifu wa viashiria hatarishi	Sababu za kibinadamu na kitamaduni (kukosa usaidizi kutoka kwa uongozi wa juu) Ukosefu wa mfumo wa kisheria na udhibiti Kukosekana kwa Miundo ya usimamizi ya kudhibiti viashiria hatarishi Ukosefu wa mfumo wa kusaidia (ICT) Kutokuwa na kiunganishi cha usimamizi wa viashiria vya hatari katika michakato ya ndani	1. Mazingira rafiki ya kudhibiti viashia vya hatari yamejumuishwa ndani ya taasisi zote (PSEs). 2. Miundo rafiki ya kiutawala kwa ajili ya kuzuia viashiria vya hatari imeimarishwa ndani ya PSEs zote. 3. Uzoefu katika usimamizi wa viashiria hatarishi umejumuishwa katika mkakati, kunanzia maandalizi na utekelezaji (mipango, bajeti na mchakato wa utendaji), na umefanyiwa mapitio na PSEs zote.
4	Uratibu mbovu na ushirikiano duni wa wasimamizi wa udhibiti	Mipangilio duni kati ya wasimaizi wa udhibiti Mapungufu katika utekelezaji	1. Mipangilio mizuri ya uratibu wa kufanya kazi kati ya wasimamizi wa udhibiti imeanzishwa.
5	Uwasilishaji duni wa ripoti za ukaguzi wa ndani kwa Kitengo cha Mkaguzi Mkuu wa Ndani (IAGD).	Kukosekana kwa mahitaji ya kisheria Mrejesho usiojitosheleza	1. Masharti ya mfumo wa kisheria juu ya uwasilishaji wa ripoti za IA kwa IAGD yameanzishwa 2. Mchakato wa IA umewekwa katika mfumo wa kimtandao ili kuhakikisha uwasilishaji wa ripoti kwa IAGD unafanyika kwa wakati. 3. Mrejesho wa kuridhisha kwa PSEs kuhusu ripoti za IA zilizowasilishwa kutolewa na kufuatiliwa na IAGD ndani ya muda mwafaka.
6	Mifumo duni ya ufuatiliaji	Kukosa utaalamu Uwajibikaji duni wa uongozi wa juu Vyanzo vya matatizo ndani ya ripoti havijaibuliwa	1. Ubora wa michakato ya IA ili kusaidia ufuatiliaji mzuri wa mapendekezo ya ukaguzi umeanzishwa. 2. Taratibu za ufuatiliaji za kimfumo za mapendekezo ya ukaguzi zimeanzishwa 3. Uwajibikaji wa watu binafsi katika PSEs kwa ufuatiliaji na utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi unaimarishwa na kuwekwa kitaasisi.

Mkakati unatoa mpango wa ujumla wa maendeleo ya mfumo wa ukaguzi wa ndani katika sekta ya umma ya Tanzania. Mafanikio ya utekelezaji wake yanakwenda pamoja na mchakato wa kina na wa muda mrefu unaotokana na midahalo ya wadau ili kuhakikisha kuwa kazi ya ukaguzi wa ndani inaambatana na viwango vya kimataifa vya ukaguzi wa ndani.[17,18]. Viwango hivi vitahitaji kubadilisha hali ya taasisi za wakaguzi wa ndani kutoka kuwa "ukaguzi kwa menejimenti" hadi "ukaguzi wa menejimenti" ambao utaimarisha kazi za uangalizi na kukomesha tabia ya kujihakiki wenyewe. Upangaji upya wa kimkakati kama huo ni utaleta changamoto kubwa itakayoathiri uhusiano uliopo wa mamlaka katika ngazi ya serikali za mitaa. Zaidi ya hayo, viwango hivyo vitapaswa kutumika nchini kwenye hatua za ugatuaji wa madaraka na usimamizi wa fedha za umma. Mkakati wa uchumi na kisiasa na muktadha wa mageuzi ulichochea mahitaji ya maoni mbalimbali kutoka kwa wadau kuhusu mawazo madhubuti ya mageuzi ili kuhakikisha kwamba hadhi ya taasisi na mwelekeo wa ukaguzi wa ndani vinaungwa mkono kwa mapana.

1.4 Malengo ya Utafiti

Madhumuni ya utafiti huu wa kazi ya ukaguzi wa ndani katika ngazi ya serikali za mitaa ni kuchangia katika mchakato wa kina na wa muda mrefu wa majadiliano ya wadau kuhusu maendeleo ya mfumo wa ukaguzi wa ndani, ili kuendana na viwango vya kimataifa vya ukaguzi wa ndani na kufikia malengo mawili ya utafiti.

1. Kulinganisha maoni ya wadau kuhusu utendaji na sifa za kazi ya ukaguzi wa ndani katika ngazi ya serikali za mitaa na viwango vya kimataifa. [19]

2. Kutoa mapendekezo kwa watunga sera kuhusu jinsi ambavyo kazi ya ukaguzi wa ndani inavyoweza kuendana na viwango vya kimataifa.

1.5 Muundo wa Ripoti

Sehemu iliyosalia ya ripoti hii imeundwa kama ifuatavyo: Sura ya pili inaelezea mbinu ya utafiti ikijumuisha maelezo ya muundo wake, mchakato wa utafiti na mapungufu. Sura ya tatu ni muhtasari wa matokeo kwa kulinganisha maoni ya wadau juu ya utendaji na sifa za kazi ya ukaguzi wa ndani ikiunganishwa na ushahidi kutoka kwenye mipango ya ukaguzi wa ndani na ripoti ambazo zilitolewa kwa watafiti. Sura ya nne inajadili matokeo yanayolenga kujibu maswali ya utafiti na kuyaweka katika muktadha wa ajenda endelevu ya mageuzi, tafiti na ripoti nyingine zilizopo. Sura ya tano inahitimisha mafanikio na changamoto zilizosalia za mchakato wa mageuzi, na Sura ya sita inatoa mapendekezo ya jinsi changamoto hizo zinavyoweza kutatuliwa.

17 Ministry of Finance and Planning and Good Financial Governance Programme (2019), Strategy for the Further Development of the Internal Audit System in the Public Sector of Tanzania, p. 21.

18 Public Finance Regulations (2004), provision 29.

19 Angalizo: Ripoti ya Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki inayohusu kazi ya Ukaguzi wa Ndani katika Sekta ya Umma Tanzania, ilitumia mbinu zinazofanana kwa kuchambua uzingatiaji wa IPPF kupitia Mbinu ya Tathmini ya Ubora ya IIA. Utafiti wa sasa, hata hivyo, unategemea zaidi mahojiano na wadau katika ngazi za serikali za mitaa na serikali kuu kubainisha maeneo yanayokubaliana na yasiyokubaliana katika utendaji, sifa za utendaji na mapendekezo madhubuti ya maboresho.

2 Mbinu za Utafiti

2.1 Maandalizi

TMaandalizi ya utafiti huu yalianza kwa kufanya mapitio ya maandiko ya sheria na kanuni husika zinazobainisha majukumu na wajibu wa wadau mbalimbali wa kazi ya ukaguzi wa ndani nchini Tanzania. Mapitio hayo yalijumuisha machapisho kuhusu mazingira mapana ya kisera kwa ajili ya uundaji wa Mkakati pamoja na maandiko mengine ya kitaalamu yakiwemo tathmini za hivi karibuni za mfumo wa usimamizi wa fedha za umma, ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, tafiti kadhaa zilizotekelezwa na Programu ya Utawala Bora wa Fedha pamoja na viwango na miongozo ya kimataifa ya ukaguzi:

- IIA, Viwango vya Kimataifa vya Mbinu za Kitaalamu za Ukaguzi wa Ndani.
- IIA, Kanuni za Maadili.
- INTOSAI GOV 9140, Uhuru wa Ukaguzi wa Ndani katika Sekta ya Umma.
- INTOSAI GOV 9150, Uratibu na Ushirikiano kati ya SAIs na Wakaguzi wa Ndani katika Sekta ya Umma.
- ISA 260, Mawasiliano na Wanaowajibika na masuala ya Utawala.
- ISA 265, Kuwasilisha Mapungufu katika Udhibiti wa Ndani kwa Wanaliopewa dhamana ya Utawala.

Mfumo wa dhana ya utafiti unafuata kwa kiasi fulani wazo la IPPF kwamba utendaji na sifa za kazi ya ukaguzi wa ndani zinahusiana. Utendaji ufanyiwa tathmini kwa kuzingatiaongezeko la thamani ndani ya taasisi. Hili linahitaji usimamizi madhubuti wa ukaguzi wa ndani kupitia upangaji unaozingatia vihatarishi, mbinu za utaratibu na nidhamu ya ushiriki wa ukaguzi, kuripoti matokeo ya ukaguzi kwa wahusika, na ufuatiliaji wa ufanisi kwa waliopewa dhamana ya kusimamia utawala. [20]

Figure 1: Dhana ya Mfumo



Utendaji huathiriwa na **sifa** za taasisi na watu wake ikiwemo shughuli za ukaguzi wa ndani, ustadi wa kada ya ukaguzi wa ndani, pamoja na uhuru wao na malengo. Uelewa wa ziada wa sifa hizi una umuhimu hasa wakati wa mazungumzo miongoni mwa wadau kuhusu rasilimali zinazohitajika ili kufadhili ushiriki wa ukaguzi, maendeleo na umahiri wa kada, pamoja na mpangilio mpya unaohitajika wa muundo wa taasisi ili kuhakikisha uhuru na kutokuwa na upendeleo kwa upande wa wakaguzi wa ndani.

Kwa kuzingatia rejea na mfumo wa dhana ya utafiti, masuala ya utendaji na sifa zinazoendana yalichaguliwa kuwa sehemu ya utafiti wa kina wa maeneo mbalimbali unaojumuisha vitengo vya ukaguzi wa ndani, kamati za ukaguzi na kamati za fedha za baraza la madiwani. Halmashauri zilichaguliwa kuunda sampuli yenye uwiano wa kijiografia ikijumuisha Arusha, Babati, Dodoma, Mbeya, Mwanza na Korogwe. Katika ngazi ya Serikali kuu, utafiti huo ulihusisha Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Kila swali la utafiti liliulizwa kwa watu wawili au zaidi kwa kutegemeana na mada husika na majukumu yao mahsusi katika mfumo wa ukaguzi wa ndani.

20 Viwango vya Utendaji 2200 na 2300 ambavyo vinashughulikia mipango na utekelezaji unaohusisha ukaguzi havikujumuishwa katika utafiti kwa sababu ufuasi wa vi wango hivi ulishapitiwa. Linganisha Programu ya Utawala Bora wa Fedha (2019), Uhakiki wa Ufuasi wa Ripoti ya Ukaguzi wa Taasisi zilizochaguliwa katika Sekta ya Umma Tanzania, Ripoti ya Mapitio ya Muda wa Kati.

Uhakiki wa ubora wa dhana ya utafiti na uchaguzi wa masuala madhubuti ya utendaji na sifa ulitolewa na Mtanzania ambaye ni mtaalamu wa ukaguzi wa ndani wa Mpango wa Utawala Bora wa Fedha. Aidha, kibali cha utafiti kilipatikana kutoka Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH), na kibali cha kufanya utafiti katika ngazi ya serikali za mitaa kilipatikana kutoka Ofisi ya Rais- TAMISEMI.

Kulingana na muundo wa utafiti, muundo wa dodoso ulitolewa kwa kila mlengwa wa mahojiano ukiwa na maswali mbalimbali; ya ndiyo au hapana (dichotomous), maswali ya kuchagua, kuweka alama ya tiki, kukadiria na yale yaliyopangiliwa kulingana na umuhimu) na maswali ya wazi. Uhakiki wa ubora ulitolewa na Mkaguzi wa Ndani aliyethibitishwa. Hojaji zilitafsiriwa kwa Kiswahili, wakati uhakiki wa ubora ulitolewa na Taasisi ya Wakaguzi wa Ndani Tanzania.

2.2 Kazi za Nje

Wakusanya takwimu walipewa mafunzo ya usimamizi wa dodoso la utafiti wakiwa na Mkaguzi wa Ndani aliyethibitishwa (Mtanzania). Baada ya mafunzo, wakusanya takwimu walifanya mahojiano na wahojiwa katika ngazi ya serikali za mitaa na serikali kuu. Lengo lilikuwa kufanya mahojiano na kila kitengo cha ukaguzi wa ndani cha Halmashauri, kamati ya ukaguzi na kamati ya fedha ya baraza la madiwani.

Jedwali 2: Sampuli ya Utafiti

Walengwa	Idadi ya Walengwa wa Usaili	Idadi halisi ya waliosailiwa
Mkaguzi wa Ndani wa Halmashauri	6	6
Kamati ya Ukaguzi ya Halmashauri	6	5
Kamati ya Fedha ya Halmashauri	6	6
Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani	1	1
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi	1	0
Ofisi ya Rais- TAMISEMI	1	0
Jumla	**21**	**18**

Wakusanya takwimu pia waliomba nakala za hadidu za rejea za vitengo vya ukaguzi wa ndani ili kutathmini wigo wao na masharti yaliyopo ili kulinda uhuru na taaluma yao. Aidha, mipango ya kazi ya mwaka ya ukaguzi wa ndani na ripoti pamoja na muhtasari wa vikao vya kamati ya ukaguzi vilitumika kutathmini upangaji wa ukaguzi wa ndani, utoaji wa taarifa na ufuatiliaji wa mchakato na kulinganisha nyaraka hizi na majibu ya utafiti. Katika Halmashauri sita, wakusanya takwimu walipata hati mbili za ukaguzi wa ndani, mipango kazi mitatu, ripoti mbili na hadidu za rejea mbili.

2.3 Uchambuzi

Hojaji zilizoandikwa kwa mkono zilitafsiriwa kutoka lugha ya Kiswahili kwenda Kiingereza na kuwekewa msimbo (code) na muundo unaoweza kusomeka kwa kompyuta. Majibu ya maswali yasiyo na mwendelezo yalichanganuliwa kwa kukokotoa makubaliano au kutokubaliana kati ya kundi lengwa la wahojiwa; maswali ya wazi yalifanyiwa uchambuzi wa ubora wa maudhui ili kutafuta dhana ya majibu ya kundi lengwa. Kisha, majibu ya wahojiwa wote wa kundi lengwa yalilinganishwa ili kuona ni wapi ambapo wadau mbalimbali wa kazi ya ukaguzi wa ndani wanakubali au kutokubaliana katika masuala ya utendaji, sifa na mapendekezo

2.4 Vikwazo

Ukubwa wa Sampuli katika ngazi ya serikali za mitaa ni ndogo kwa sababu ya uhaba wa rasilimali za utafiti. Kwa sababu hiyo, matokeo yanapaswa kufasiriwa kama utafiti ama uchunguzi wenye madhumuni ya kutambua masuala ya sifa (kutofautiana na viwango vya kimataifa) ambayo inaweza kuelezea kwa kiasi masuala ya utendaji; lakini matokeo ya utafiti hayawezi kuchukuliwa kama yaliyofikia hatua ya mwisho. Licha ya udogo wa sampuli, utafiti unaweza kubainisha maeneo ya kukubaliana ama kutokubaliana miongoni mwa wadau. Maeneo ambayo wadau wanakubaliana kwa kiasi kikubwa yanaweza kupitishwa kuwa sehemu ya Mkakati, lakini maeneo ambayo wadau wamekubaliana kwa kiasi kidogo yanaweza kufanyiwa utafiti zaidi na kuendelea kufanyika kwa mijadala ya kina ya wadau.

Katika ngazi ya serikali za mitaa, walengwa wote walihojiwa walijibu maswali ya utafiti isipokuwa kamati moja ya ukaguzi. Katika ngazi ya serikali kuu, Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani ilishiriki katika utafiti huo, lakini Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi na Ofisi ya Rais TAMISEMI hazikujibu maombi ya usaili. Kukosekana kwa ushiriki wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kunamaanisha kwamba maoni muhimu kuhusu wakaguzi wa nje, uhuru na malengo ya wakaguzi wa ndani hayakupatikana, mambo ambayo ni muhimu katika kubainisha iwapo wakaguzi wa nje wanaweza kuratibu na kushirikiana na wakaguzi wa ndani, na kwa kiasi gani wanaweza kutumia kazi ya wakaguzi wa ndani kuhakikisha shughuli zinafanyika kwa namna inayofaa na kupunguza kurudiarudia kazi.[21] Kukosekana kwa ushiriki wa Ofisi ya Rais TAMISEMI kunamaanisha kwamba kuna uelewa mdogo wa namna Wizara inavyopokea na kufuatilia mawasiliano kutoka kwa wakaguzi wa ndani, kuhusu mapungufu makubwa katika udhibiti wa ndani. Jambo hili linaweza kutilia shaka uadilifu au uwezo wa menejimenti ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Ingependeza kujua pia jinsi Wizara inavyoshughulikia kesi, pale ambapo menejimenti ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa inapokiri kwamba kuna vihatarishi ambavyo havikubaliki ndani ya taasisi.

21 INTOSAI 9150, Sehemu ya 2.1.

3 Matokeo

3.1 Kuongeza Thamani

Kwa mujibu wa Taasisi ya Wakaguzi wa Ndani, madhumuni ya shughuli ya ukaguzi wa ndani ni kuongeza thamani na kuboresha shughuli za taasisi. Hii inahitaji shughuli ya ukaguzi wa ndani kuzingatia malengo, mikakati na vihatarishi wakati inapotoa huduma za uhakiki na ushauri kwa taasisi husika.

Je, kazi ya ukaguzi wa ndani inaongeza thamani kwa taasisi na wadau wake?

Wahojiwa wote katika ngazi ya serikali za mitaa na serikali kuu walikubaliana kuwa manufaa ya kazi ya ukaguzi wa ndani yanazidi gharama za mfumo wa usimamizi wa fedha za umma kwa ujumla.

Swali moja la kimkakati kwa maendeleo ya kazi ya ukaguzi wa ndani ni malengo gani ya usimamizi wa fedha ya umma ambayo inapaswa kuzingatia ili kuongeza thamani kwa taasisi. Baadhi ya nchi huweka udhibiti mkali ili kuhakikisha nidhamu ya fedha na ufuasi wa sheria, huku nchi nyingine zikiruhusu unyumbufu zaidi wa usimamizi ili kuchochea utendaji bora wa kazi katika utoaji wa huduma za umma. Waliohojiwa wengi katika ngazi ya serikali za mitaa waliainisha kuwa kazi ya ukaguzi wa ndani ina malengo mawili kwa usimamizi wa fedha za umma 'uaminifu katika hesabu za mwaka na ufuasi wa taratibu' na 'ufanisi na usahihi', wakati 'nidhamu ya fedha' ilionekana kuwa na matatizo kidogo. Maoni ya pamoja yalikuwa kwamba kazi ya ukaguzi wa ndani inazingatia malengo sahihi ya usimamizi wa fedha za umma. Kazi ya ukaguzi wa ndani pia inahitaji kuelekeza rasilimali zake kwenye maeneo yenye vihatarishi. Kitengo cha Mkaguzi Mkuu wa Ndani (IAGD) na wakaguzi wengi wa ndani (3 kati ya 5 waliojibu) walikubaliana kuwa 'tathmini ya mifumo ya udhibiti wa ndani, usimamizi wa vihatarishi na mifumo ya utawala', 'malipo ya mishahara na usimamizi wa rasilimali watu' pamoja na 'manunuzi na mikataba' ni miongoni mwa maeneo matano ya kipaumbele ya vihatarishi (linganisha Jedwali la 3 hapo chini).

Ingawa maoni yao kuhusu vipaumbele vya maeneo mengine yanayohitaji tahadhari yalitofautiana, IAGD na wakaguzi wengi wa ndani pia walikubaliana kwamba kuangazia upya rasilimali za ukaguzi wa ndani kwenye 'usimamizi wa mali' kungeongeza thamani ya juu zaidi. Kwa bahati mbaya, wakaguzi wengi wa ndani walitathmini kwamba utumishi na utaalamu unaopatikana katika maeneo yote ya vihatarishi hautoshi. Hii inatumika hasa kwa 'tathmini ya maendeleo na miradi mingineyo' pamoja na 'usimamizi wa ununuzi na mikataba'. Pale ambapo kuna uhaba wa wafanyakazi, tunaweza kusema kwamba uendelezaji wa kada mahiri ya ukaguzi wa ndani uko makini hasa pale unaposimamiwa na serikali kuu ili kuepusha wafanyakazi kulazimishwa kufanya shughuli nyingi tofauti, na hivyo kupunguza umakini kazini.[22] Hata hivyo, wahojiwa wengi walikataa wazo la kuunda timu maalum za serikali kuu kufanya ukaguzi maalum kwa sababu timu hizi zitaongeza gharama, kusababisha kazi kurudiwa mara mbili, au hazitaweza kujibu kwa wakati mahitaji ya kila siku. Kulingana na IGAD, miongozo hiyo inaruhusu kutafuta wataalam wengine ikiwa hakuna afisa aliye na ujuzi unaohitajika.

22 Allen, Hemming, Potter (2013), The International Handbook on Public Financial Management, p. 385.

Jedwali Na. 3: Kurekebisha Uzoefu wa kazi kwa maeneo ya kipaumbele yenye vihatarishi

Eneo la kipaumbele vya vihatarishi	**Maeneo makuu 5** ya tahadhari kwa sasa? *(Uthibitisho)*		Vipaumbele vyenye **ongezeko la juu la thamani?** *(Uthibitisho)*		**Wafanyakazi** wa kutosha **na utaalamu?**
	IAGD	Wakaguzi wa Ndani	IAGD	Wakaguzi wa Ndani	Wakaguzi wa Ndani
Maandalizi na utekelezaji wa bajeti	Hapana	60%	Hapana	20%	30%
Tathmini ya mfumo wa udhibiti wa ndani, usimamizi wa vihatarishi, mfumo wa utawala	Ndiyo	60%	Hapana	40%	20%
Mishahara na usimamizi wa rasilimali watu	Ndiyo	60%	Hapana	0%	20%
Tathmini ya Maendeleo na miradi mingine	Ndiyo	20%	Hapana	20%	0%
Manunuzi na Usimamizi wa Mikataba	Ndiyo	100%	Hapana	20%	0%
Usimamizi wa Matumizi	Ndiyo	20%	Hapana	0%	20%
Usimamizi wa Mapato	Hapana	60%	Ndiyo	0%	20%
Usimaizi wa mali	Hapana	20%	Ndiyo	60%	20%
Ufuatiliaji wa mapendekezo ya mkaguzi wa nje	Hapana	60%	No	0%	20%

Je, kazi ya ukaguzi wa ndani inazingatia mchango wa wasimamizi wakuu?

Kwa mujibu wa kiwango cha utendaji cha IPPF 2010.A1, wakaguzi wa ndani lazima waandae mpango wa ukaguzi wa kila mwaka unaozingatia tahadhari kulingana na malengo ya taasisi, na maoni ya wasimamizi wakuu na bodi lazima yazingatiwe katika mchakato huu.

Licha ya maoni kutoka kwa kamati ya usimamizi na ukaguzi ya Halmashauri, wakaguzi wengi wa ndani waliohojiwa pia hupokea maoni kutoka kwa mamlaka zingine za serikali, kama vile IAGD na CAG, na kwa kawaida maoni yao huendana na tathmini iliyoandikwa ya vihatarishi kutoka Mamlaka ya Serikali ya Mitaa. Hata hivyo, inaweza kujitokeza hali ambapo maoni hayo yakawa ni kipaumbele cha serikali kuu na sio cha ngazi ya chini. Wakaguzi wote wa ndani (6 kati ya 6 waliojibu) na wajumbe wa kamati ya ukaguzi (wanne kati ya 4 waliojibu) waliunga mkono wazo kwamba afisa mratibu wa viashiria hatarishi wa Halmashauri anapaswa kutoa ushauri katika hali hiyo kama shughuli iliyopendekezwa inaendana na tahadhari za halmashauri, na hivyo basi zipate ufadhili wa Halmashauri husika; lakini IAGD haikutoa maoni kama haya.

Je, kazi ya ukaguzi wa ndani inatoa huduma za ushauri ili kuimarisha utawala, usimamizi wa maeneo ya vihatarishi na michakato ya udhibiti?

Kiwango cha utendakazi cha IPPF 2100 kinasisitiza kwamba kazi ya ukaguzi wa ndani iongeze thamani kwa kutoa huduma za ushauri ili kuimarisha usimamizi, michakato ya udhibiti wa vihatarishi vinavyoweza kujitokeza, na udhibiti wa shughuli za ndani ya taasisi. Huduma ya ushauri - kama vile kwa baraza la madiwani, uwezeshaji na mafunzo kwa kawaida hufanyika kutokana na ombi maalum la mteja husika.

Wakaguzi wote wa ndani waliohojiwa walithibitisha kuwa wanatoa huduma za ushauri ili kuimarisha usimamizi wa taasisi, udhibiti wa maeneo yenye vihatarishi na michakato ya udhibiti. Wateja wao wakuu katika ngazi ya serikali za mitaa ni kamati ya ukaguzi na kamati ya fedha; mteja mkuu katika ngazi ya serikali kuu ni IAGD na

wakati mwingine pia OR-TAMISEMI au Sekretarieti ya Mkoa. Wakaguzi wa ndani na IAGD pia walithibitisha kuwa Programu ya Marekebisho ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Kamati ya Uongozi ya Pamoja na ile ya Utekelezaji ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa zote zinajadili matatizo katika utawala, usimamizi wa vihatarishi na michakato ya udhibiti, na wanatoa mapendekezo ya kimkakati ambapo kazi ya ukaguzi wa ndani inaweza kuongeza thamani ya shughuli za serikali kwa kutoa huduma za ushauri.

Je, kazi ya ukaguzi wa ndani inafanya uhakiki kwa ukamilifu?

Kiwango cha utendaji cha IPPF 2420 kinaeleza kuwa ripoti za ukaguzi wa ndani lazima ziwe na matokeo ya tathmini yenye ukweli na inayoendana sawa na mazingira husika. Aidha, kiwango cha utendaji cha IPPF 2440. A1 kinawataka wakaguzi wa ndani kuwasilisha matokeo ya ukaguzi kwa wahusika wanaoweza kuthibitisha kwamba matokeo ya kazi zao yanazingatiwa.

Wakaguzi wa ndani na IAGD wote walikubaliana kuwa ripoti za ukaguzi wa ndani kwa ujumla hutoa tathmini sawia, yenye ukweli na inayoendana na mazingira husika. Pia, walithibitisha kuwa Mwongozo wa Ukaguzi wa Ndani na Kielelezo cha Kuripoti vinashughulikia mamlaka inayohusika katika ngazi ya serikali ya mitaa au serikali kuu ambayo inawajibika kama chanzo na msingi wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi.

Hata hivyo, mazingira ya Halmashauri pia yanaweza kuwa chanzo cha udhibiti dhaifu. Kwa mfano, uchambuzi wa taarifa za ukaguzi wa ndani unaonesha hoja juu ya kushindwa kutumia 2% (asilimia mbili) ya fedha zilizopokelewa kutekeleza shughuli za maendeleo kinyume na Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Zaidi ya hayo, ripoti inapendekeza kupitiwa upya kwa bajeti ili kufikiria utekelezaji wa vipengele vya bajeti, na halmashauri inapaswa kutoa fedha zilizoidhinishwa bila kuchelewa. Lakini ripoti hiyo haijataja kuwa asilimia 47 ya fedha za bajeti hazikupokelewa kutoka kwa serikali kuu na wafadhili wa miradi, na hivyo kuvuruga utoaji wa huduma kwa walengwa. Mfano huu unaonesha kuwa utambuzi na kushughulikia vyanzo vya tatizo katika ngazi ya serikali kuu - ambayo ni sehemu ya Halmashauri - kunaweza kuhitaji uangalizi wa kina kutoka kwa wakaguzi wa ndani.

3.2 Mipango

Ukaguzi wa ndani unaochukua tahadhari kwa vihatarishi huipa taasisi uhakika kwamba kuna ufanisi katika udhibiti. Ili kufanya kazi hii, mkaguzi wa ndani anahitaji rasilimali za kutosha ili kukamilisha mpango. Zaidi, wakaguzi wa ndani na wa nje wanapaswa kuratibu kazi zilizopangwa ili kuhakikisha zinashughulikiwa kwa umakini unaokubalika kimataifa na kupunguza kujirudia rudia kwa kazi.

Je, kazi ya ukaguzi wa ndani inatumia mipango kazi inayozingatia vihatarishi?

Kiwango cha utendaji cha IPPF 2010.A1 kinahitaji mipango ya ukaguzi wa ndani kuzingatia tathmini ya vihatarishi inayofanywa angalau kila mwaka.

Wakaguzi wengi wa ndani waliohojiwa na wajumbe wa kamati za ukaguzi walikubaliana kuwa mipango ya ukaguzi wa ndani inategemea rejista za vihatarishi zilizopo. Pia walikubaliana kuwa majukumu ya msimamizi wa vihatarishi katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa yamefafanuliwa wazi na kwamba wanawajibishwa; lakini mambo yaliyo nje ya mamlaka yao, kama vile ukosefu wa rasilimali pamoja na masuala ya kimfumo na ushawishi wa kisiasa huathiri utendakazi wa afisa mratibu wa vihatarishi. Wakaguzi wa ndani na wajumbe wa kamati za ukaguzi wote walisisitiza kuwa maafisa wasimamizi wa vihatarishi wanahitaji kujengewa uwezo zaidi. Kwa vile Halmashauri hazina rasilimali zinazohitajika kwa shughuli hiyo, kamati za ukaguzi zilipendekeza mafunzo hayo yatolewe na wataalamu kutoka ofisi ya Sekretarieti ya Mkoa.

Je, kazi ya ukaguzi wa ndani ina rasilimali za kutosha?

Kiwango cha utendaji cha IPPF 1130 kinaeleza kuwa uhuru wa shughuli ya ukaguzi wa ndani unaweza kukumbwa na vikwazo kutokana na ama mwonekano wake, kukosekana kwa taarifa sahihi au inapotokea ukomo wa rasilimali, kwa mfano fedha. Kiwango cha utendaji 1110 kinamtaka mkaguzi wa ndani kuweka wazi vikwazo hivyo kwa bodi na kujadili athari zake. Bodi inapaswa kufanya uchunguzi unaostahili wa usimamizi ili kubaini kama kuna changamoto au mapungufu ya rasilimali.

Mahojiano na wakaguzi wa ndani na wajumbe wa kamati za ukaguzi yalionesha kukubaliana kwa mapana kuwa vitengo vya ukaguzi wa ndani havina ufadhili wa kutosha, na walikadiria uhaba wa fedha uliopo kati ya 40% na 50%. Baadhi ya wajumbe wa kamati ya ukaguzi (2 kati ya 5 waliojibu) waliripoti kuwa ufinyu wa rasilimali wakati mwingine husababisha wigo mfinyu wa ukaguzi, jambo ambalo linaweza kusababisha kurudiwa rudiwa kwa kazi kwani mkaguzi wa nje pia anakagua eneo lile lile na tena matokeo yao yanayofanana

sana. Kamati ya ukaguzi na wajumbe wa kamati ya fedha walithibitisha kuwa mkaguzi wa ndani anawasilisha athari za upungufu wa rasilimali, na kamati za fedha hufanya uchunguzi kujiridhisha iwapo mapungufu hayo yanastahili kuwepo.

Mwongozo wa Shirika la Kimataifa la Taasisi Kuu za Ukaguzi wa utawala bora INTOSAI Gov 9140 kuhusu Uhuru wa Ukaguzi wa Ndani katika Sekta ya Umma unapendekeza kwamba hitaji la kisheria la kuanzisha shughuli ya ukaguzi wa ndani husaidia kulinda ufadhili na uhuru wake.

Wajumbe wa kamati za ukaguzi na kamati za fedha wote walithibitisha kuwa kitengo cha ukaguzi wa ndani kina mamlaka ya kisheria yenye madhumuni ya wazi, na mpango mkakati wa halmashauri unajumuisha malengo, na bajeti maalum ('kifungu') kwa ukaguzi wa ndani. Miongozo ya mipango na bajeti ni pamoja na masharti inajumuisha vipengele vinavyohakikisha kwamba kuna ufadhili wa kutosha; hata hivyo, mjumbe mmoja wa kamati ya ukaguzi alikiri kwamba masharti hayo hayafuatwi wakati wote. Wakaguzi wawili wa ndani walisema kwamba ukomo wa bajeti ni mdogo sana, na Makatibu Wakuu wa Hazina na Ofisi ya Rais TAMISEMI wanapaswa kupitia upya ukomo wa bajeti.

Je, kazi ya ukaguzi wa ndani inaratibu shughuli zake na kazi ya ukaguzi wa nje?

Kiwango cha utendaji cha IPPF 2050 kinasema kwamba wakaguzi wa ndani wanapaswa kutoa taarifa, kuratibu shughuli, na kuzingatia kazi za watoa huduma wengine wa ndani na nje na watoa huduma za ushauri ili kuhakikisha kwamba wameshughulikia maeneo yote na kupunguza marudio ya kazi. Wakaguzi wa ndani walieleza kuwa mara kwa mara wanatoa ripoti zao kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Pia kuna miongozo na taratibu zinazowaruhusu wakaguzi wa nje kushiriki katika vikao vya kamati ya ukaguzi, lakini ni baadhi tu ya wakaguzi wa ndani hukutana mara kwa mara na wajumbe wa ukaguzi wa nje ili kujadili ripoti zao na kuepuka marudio. Pia walieleza kuwa wajumbe wa kazi ya ukaguzi wa ndani na nje hawashiriki mafunzo au kubadilishana wafanyakazi.

INTOSAI GOV 9150 inaelezea kuhusu Uratibu na Ushirikiano kati ya Taasisi Kuu za Ukaguzi (SAIs) na Wakaguzi wa Ndani katika Sekta ya Umma kwamba uhuru na kutopendelea kwa mkaguzi wa ndani ni mambo muhimu ya kuzingatiwa na wakaguzi wa nje wakati wa kubaini iwapo wataweza kuratibu na kushirikiana na mkaguzi wa ndani, na ni kwa kiwango gani wanaweza kutumia kazi ya mkaguzi wa ndani. [23] Taasisi zote mbili za ukaguzi wa juu (nchini Tanzania, yaani CAG) na wakaguzi wa ndani wana viwango vyao vya vinavyojitegemea. Kiwango cha utendaji cha IPPF 1100 kinahitaji shughuli ya ukaguzi wa ndani kuwa huru na bila upendeleo, ambayo inahitaji mkaguzi wa ndani kuweza kuwafikia moja kwa moja wasimamizi wakuu na bodi bila vikwazo . Kiwango cha utendaji 1110 kinamtaka mkaguzi wa ndani kuripoti kiutendaji kwa bodi, na lazima aithibitishie bodi, angalau kila mwaka, uhuru wa shughuli ya ukaguzi wa ndani wa taasisi.

Kwa muktadha wa Tanzania, 'bodi' ndiyo baraza la madiwani kupitia kamati yake ya fedha, yenye jukumu la kudhibiti na kusimamia fedha za Halmashauri. Wakati wa mahojiano, wakaguzi wengi wa ndani walithibitisha uwepo wa uhuru wao kama taasisi, wanapokutana na kamati ya fedha. Dai hili lilithibitishwa tena na wajumbe wengi wa kamati za fedha.

3.3 Kushiriki katika Ukaguzi

Ushiriki wa ukaguzi lazima ufanywe kwa kuzingatia Mfumo wa Kimataifa wa Uzoefu wa Kitaaluma (IPPF), na lazima usimamiwe ipasavyo ili kuhakikisha kuwa malengo ya ukaguzi yanafikiwa, ubora unahakikiwa, na wafanyikazi wanaendelezwa.

Je, kazi ya ukaguzi wa ndani inapata ushauri na usaidizi unaofaa kulingana na viwango vya kimataifa?

Kiwango cha 1210 cha sifa ya IPPF kinahitaji kwamba kazi ya ukaguzi wa ndani kwa pamoja iwe na maarifa, ujuzi, na uwezo mwingine au kupata ushauri na usaidizi mahiri ili kutekeleza majukumu yake yote au sehemu ya shughuli zake.

Mwaka 2016, Mkaguzi Mkuu wa Ndani alitoa Kitabu cha Ukaguzi wa Ndani kilichorekebishwa na Mwongozo wa Ukaguzi wa Ndani ('Kitabu cha Mwongozo') kama nyongeza ya Mwongozo wa Ukaguzi wa Ndani, ili kusaidia kuongoza mchakato wa ukaguzi wa ndani. Miongozo yote hii inafungamana na IPPF na sheria na kanuni za Tanzania. Wakaguzi wote wa ndani waliohojiwa walithibitisha kwamba wanatumia miongozo hiyo kwa pamoja 'mara nyingi', na karibu wote walizingatia kiwango cha uwezo wao kama 'wataalamu', na mmoja

23 INTOSAI GOV 9150, Sehemu ya 2.1.

tu kati yao alikuwa 'mgeni'. Kiwango cha 1322 cha sifa ya IPPF kinahitaji wakaguzi wa ndani kuweka wazi iwapo kutofuatwa kwa IPPF na wasimamizi wakuu na bodi, kutaathiri wigo wa uendeshaji wa shughuli ya ukaguzi wa ndani.

Wajumbe wote wa kamati za ukaguzi na wajumbe wengi wa kamati za fedha walithibitisha wakati wa mahojiano kwamba wakaguzi wa ndani walifichua kutofuatwa kwa IPPF. Pia wanatoa mipango ya kushughulikia masuala muhimu ya kutozingatiwa kwa IPPF. Hata hivyo, ujuzi wa kutosha wa IPPF si hitaji la msingi la ufaulu wakati wa kuajiri wakaguzi wa ndani. Ingawa IAGD na wajumbe wengi wa kamati ya ukaguzi waliunga mkono maoni kwamba ujuzi huo unapaswa kuwa hitaji au sifa ya msingi, wakaguzi wa ndani hawakukubaliana na wakapendekeza kuwa IPPF iwe sehemu ya mtaala wa wahasibu. Wakaguzi wa ndani pia walipendekeza kuwe na mafunzo ya kujiendeleza kazini na kujenga uwezo ili kuhakikisha kuwa wanafahamu mabadiliko yanayoendelea katika viwango vya IPPF. IAGD pia ilitoa maoni kama hayo.

Je, kuna changamoto katika kufikia malengo ya ushiriki wa ukaguzi?

Kiwango cha sifa ya IPPF 1130 kinaeleza kuwa mipaka ya wigo; ufikiwaji mdogo wa rekodi, wafanyakazi, na mali; au ukomo wa rasilimali, kama vile ufadhili, vinaweza kudhoofisha uhuru au kutopendelea kwa upande wa mkaguzi wa ndani, na ni lazima wafichue vikwazo hivyo kwa ngazi husika. Wakaguzi wengi wa ndani waliohojiwa walipata changamoto katika kufikia malengo ya ushiriki kwenye ukaguzi kutokana na uhaba wa wafanyakazi, fedha na matumizi ya analojia yanayochukua muda mrefu kwani shughuli nyingi hazitumii programu za kompyuta. Wakaguzi wengi wa ndani walithibitisha kuweza kufikia mali na rekodi za wafanyikazi bila vikwazo. Hata hivyo, moja ya ripoti ya ukaguzi wa ndani iliyochambuliwa ilionesha kuwa nyaraka tano ziliombwa lakini hazikuwasilishwa kwa madhumuni ya ukaguzi na kusababisha ionekane kwamba kuna ukomo wa wigo.

Ugumu ambao mara nyingi unazuia utekelezaji mzuri wa mipango ya ukaguzi ni jinsi ya kushughulikia dharura (shughuli zilizo nje ya mpango). Kwa kawaida maombi hayo hutumwa kwa afisa anayehusika na kamati ya ukaguzi kwa ajili ya kujadiliwa na kuidhinishwa kabla ya kuunganishwa katika mpango kazi wa ukaguzi wa ndani. Si mamlaka zote zinatoa ufadhili kwa shughuli za dharura, hivyo basi, baadhi ya shughuli zinashindwa kutekelezwa kikamilifu. Wakati mipango miwili kati ya mitatu ya ukaguzi wa ndani iliyochambuliwa haitoi muda kwa ajili ya shughuli za dharura, mpango wa tatu una 'posho ya dharura' ikiwa ni pamoja na asilimia tano kwa siku za kazi.

Wajumbe wa kamati za fedha walithibitisha kuwa wakaguzi wa ndani waliwasilisha matatizo yote makubwa waliyokumbana nayo wakati wa ukaguzi, na madiwani walidai kuwa walifanya uchunguzi unaostahili kwa menejimenti na mkaguzi mkuu wa ndani ili kubaini iwapo wigo wa kazi una vikwazo vyovyote. Mkaguzi mmoja wa ndani na mjumbe wa kamati ya ukaguzi walieleza kuwa, mapungufu ya wigo yanaweza kupelekea marekebisho ya maoni ya mkaguzi, lakini hayawezi kuwa sababu ya kuondolewa kwenye ukaguzi.

Je, kuna changamoto katika uhakiki wa ubora?

Kiwango cha 1300 cha sifa ya IPPF kinahitaji utendakazi wa ukaguzi wa ndani ili kuunda na kudumisha programu ya uhakiki wa ubora na uboreshaji wa program ambayo inashughulikia vipengele vyote vya shughuli ya ukaguzi wa ndani. Programu lazima ijumuishe tathmini za ndani na nje. Tathmini ya ndani inapaswa kuwa sehemu ya ufuatiliaji na usimamizi na uingizwe katika sera na uzoefu wa kusimamia shughuli za ukaguzi wa ndani. Tathmini ya nje inapaswa kujumuisha maoni ya kiutendaji na ya kimkakati na kufanywa na mtathmini wa nje aliyeidhinishwa (nchini Tanzania, tathmini ya nje hufanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali). Mkaguzi wa ndani lazima awasilishe matokeo ya tathmini ya ndani na nje ikiwa ni pamoja na hitimisho na mipango iliyorekebishwa kwa menejimenti na bodi.

Mwaka 2018, Programu ya Utawala Bora wa Fedha ilitengeneza Zana ya Kujisimamia ili kuhakikisha kuwa kazi zinalingana na IPPF. Wakati wa mahojiano, wakaguzi wote wa ndani walieleza kuwa wanatumia Zana ya Kujifuatilia 'mara nyingi'. Changamoto inayojitokeza zaidi ya ufuatiliaji na usimamizi wa ndani kwa wafanyakazi wa ukaguzi wa ndani ni mzigo mkubwa wa kazi ya msimamizi ikifuatiwa na changamoto za zana za usimamizi na mchakato wa usimamizi. Maoni mengi ya kiutendaji na ya kimkakati kutoka kwa tathmini ya nje yametekelezwa, lakini ukosefu wa rasilimali unazuia utekelezaji wake kikamilifu. Matokeo ya tathmini ya ndani na nje ikiwa ni pamoja na hitimisho na marekebisho ya mipango, mara zote huwasilishwa kwa kamati ya ukaguzi na mara nyingi (4 kati ya 6) kwa kamati ya fedha na Mkaguzi Mkuu wa Ndani.

Je, kuna changamoto katika maendeleo ya wafanyakazi?

Kiwango cha 1210 cha sifa ya IPPF kinaeleza kuwa wakaguzi wa ndani wanahimizwa kuonesha ustadi wao kwa kupata vyeti na sifa zinazofaa za kitaaluma, kama vile cheo cha Mkaguzi wa Ndani Aliyeidhinishwa (CIA) na nyadhifa zingine zinazotolewa na Taasisi ya Wakaguzi wa Ndani na mashirika mengine ya kitaaluma. Miongoni mwa wakaguzi wa ndani waliohojiwa, ni wachache tu waliokuwa wameidhinishwa kama (CIA), wengi wao walikuwa ni wahasibu walioidhinishwa (CPA). Wengi wao hawakupata cheti cha CIA - hasa kwa sababu halikuwa sharti, na nusu yao wanafanya kazi kama mkaguzi wa ndani katika sekta ya umma kwa sababu mahitaji ya kazi ni kuwa mhasibu na ukaguzi ni sehemu tu ya mtaala wa uhasibu. Mkaguzi mmoja wa ndani alishauri kwamba kuna haja ya mabadiliko.

Wakaguzi wote wa ndani walionesha kuwa uhaba wa fedha ndio changamoto kubwa ya kuboresha ustadi wao kupitia programu endelevu za kuendeleza wafanyikazi. Wakati Mamlaka za Serikali za Mitaa zikitumia rasilimali zao kukuza maendeleo ya wafanyakazi, IAGD na OR-TAMISEMI pia hutoa programu za mafunzo zinazofadhiliwa, hasa pale zinapoanzisha mifumo mipya ya udhibiti wa ndani katika ngazi ya serikali za mitaa. Wakaguzi wengi wa ndani walikubali kuwa mchakato wa ukuzaji wa taaluma unahusishwa na mahitaji yao ya mafunzo binafsi, lakini pia wanasema kuwa hakuna mchakato wa ufuatiliaji na tathmini ya mafunzo. [24]

3.4 Utoaji taarifa

Wakaguzi wa ndani lazima waripoti matokeo ya shughuli za ukaguzi kikamilifu na kwa wakati kwa pande zinazohusika ambazo zinaweza kuhakikisha kuwa matokeo yanazingatiwa ipasavyo.

Je, matokeo ya ushiriki wa ukaguzi yanawasilishwa kwa ukamilifu na kwa wakati?

Kiwango cha utendaji cha IPPF 2060 kinahitaji wakaguzi wa ndani kuripoti mara kwa mara kwa menejimenti na bodi. Kiwango kinaeleza mara ngapi inapaswa kuripoti na maudhui ya kuripoti huamuliwa kwa ushirikiano na mkaguzi mkuu wa ndani, menejimenti na bodi. Wajumbe wengi wa kamati za ukaguzi na kamati za fedha walithibitisha kuwa wakaguzi wa ndani kwa ujumla huwasilisha ripoti zao za ukaguzi kwa wakati kulingana na ratiba iliyopangwa. Ripoti za robo mwaka na za mwaka zinapaswa kuwasilishwa siku 15 baada ya mwisho wa robo au mwaka kwa mtendaji mkuu (DED) ili zitumwe kwa kamati ya fedha ya baraza la madiwani.

Nakala za ripoti hizo hutumwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Mkaguzi Mkuu wa Ndani, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Sekretarieti ya Mkoa. [25] Ikiwa ripoti za ukaguzi wa ndani hazitawasilishwa kwa wakati, kwa kawaida ni kwa sababu ya masuala ya kibajeti ambayo huchelewesha utekelezaji wa shughuli za ukaguzi wa ndani zilizopangwa. Wakaguzi wengi wa ndani waliohojiwa walikubali kwamba wanapaswa kuwa na mamlaka ya kuwasilisha ripoti ya ukaguzi wa ndani kwa kamati ya fedha ikiwa majibu ya menejimenti yanacheleweshwa bila sababu za msingi.

Je, kuna muhtasari wa ripoti ya uchunguzi na mapendekezo juu ya ukaguzi?

Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2010 inamtaka Mkaguzi Mkuu wa Ndani kuchunguza na kukusanya taarifa za ukaguzi kutoka kwa mamlaka za umma na miradi inayofadhiliwa na wafadhili na kuandaa ripoti ya muhtasari yenye uchunguzi na mapendekezo makuu ya ukaguzi. Kitengo cha Mkaguzi Mkuu wa Ndani kilieleza wakati wa mahojiano kuwa wanatoa ripoti ya muhtasari kutokana na taarifa za ukaguzi wa ndani kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa. Lakini utayarishaji wa ripoti za muhtasari unakuwa mgumu kutokana na kuchelewa kuwasilishwa kwa baadhi ya ripoti na kutofuata miundo na viwango vilivyowekwa.

Muhtasari wa ripoti unajumuisha majibu na hatua zinazopaswa kuchukuliwa na mamlaka za serikali kuu, lakini baadhi ya mamlaka za serikali kuu huwasilisha maoni yao kwa kuchelewa, na wakati mwingine hakuna mrejesho wowote.

Je, kitengo cha ukaguzi wa ndani kinawasilisha matokeo kwa wahusika?

Kiwango cha sifa cha IPPF 1110.A1 kinahitaji kwamba shughuli ya ukaguzi wa ndani lazima iwe huru, bila kuingiliwa katika kubainisha wigo wa ukaguzi wa ndani, kufanya kazi na kuwasilisha matokeo.

24 Moja kati ya mipango mitatu ya ukaguzi wa ndani iliyochambuliwa inatenga 19% ya bajeti ya kitengo cha ukaguzi wa ndani kwa ajili ya maendeleo ya wafanyakazi, wakati mipango mingine miwili inatenga wiki mbili za mafunzo kwa kila mkaguzi wa ndani (haijumuishi makadirio yoyote ya bajeti). Aidha, hati moja ya ukaguzi wa ndani iliyochambuliwa inamtaka Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi kuendelea kuwasiliana na Mkaguzi Mkuu wa Ndani kwa ajili ya zoezi la tathmini ya utumishi, mahitaji ya watumishi, mafunzo, na maendeleo ya kiufundi na kitaaluma.

25 Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa (2009), Sehemu ya 14.

Wakaguzi wengi wa ndani waliohojiwa walieleza kuwa katika taaluma yao 'hawajawahi' kujikuta wakielekezwa kukandamiza, au kurekebisha kwa kiasi kikubwa, matokeo halali ya ukaguzi wa ndani au ripoti. Ni baadhi tu ya wakaguzi wa ndani waliopata usumbufu kama huo, na ni mara chache.

Kiwango cha 1100 cha sifa ya IPPF kinaeleza kuwa uhuru wa taasisi unaweza kupatikana kupitia uhusiano wa ripoti mbili ambapo mkaguzi mkuu wa ndani anaripoti kiutawala kwa menejimenti ya juu na kiutendaji kwa bodi. Wakaguzi wa ndani wana uhusiano wa kuripoti mara mbili: wanaripoti kiutawala kwa mtendaji mkuu, ambaye pia ni mkurugenzi mtendaji wa LGA; lakini wanaripoti kiutendaji kwa kamati ya ukaguzi na Mkaguzi Mkuu wa Ndani [26] na si kwa bodi/chombo cha uangalizi cha Halmashauri.

Wakaguzi wote wa ndani waliohojiwa na wajumbe wote wa kamati za fedha waliunga mkono wazo kwamba mkaguzi wa ndani anapaswa kuripoti kwa kamati ya fedha ya halmashauri. Lakini wajumbe wengi wa kamati za ukaguzi hawakuunga mkono wazo hilo; mmoja wao alieleza kuwa inaweza kusababisha kutoelewana kati ya uongozi wa halmashauri na kamati ya fedha.

Je, mkaguzi wa ndani anaalikwa kuhudhuria mikutano mara kwa mara?

Kufuatia Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA) 260 (na Marekebisho) kuhusu Mawasiliano na Wale Walipewa mamlaka ya Utawala, kanuni za utawala bora zinapendekeza kuwa mkaguzi anatakiwa kualikwa kuhudhuria mara kwa mara mikutano na wenye mamlaka ya utawala, ambayo inapaswa pia kukutana na mkaguzi wa ndani bila uwepo wa menejimenti, angalau kila mwaka.[27]

Wadau wote katika ngazi ya serikali za mitaa walithibitisha kuwa mkaguzi mkuu wa ndani anaalikwa kuhudhuria mara kwa mara vikao vya kamati ya ukaguzi na kamati ya fedha. Hadidu za rejea za kamati ya ukaguzi zinahitaji kukutana na mkaguzi wa ndani bila uwepo wa menejimenti. Lakini kamati ya fedha ya halmashauri haikutani na mkaguzi wa ndani bila uwepo wa menejimenti, na wadau wengi wa serikali za mitaa wanafikiri kwamba hali hiyo haipaswi kubadilika. Hata hivyo, wakaguzi wengi wa ndani walikubali kwamba waalikwe kuhudhuria mikutano katika ngazi ya serikali kuu ili kujadili masuala (kama vile sababu za msingi na hatua zinazopaswa kuchukuliwa na mamlaka za serikali kuu).

Je, mapungufu katika udhibiti wa ndani yanawasilishwa kwa ngazi husika ya menejimenti?

Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA) 265 vinamtaka mkaguzi kuwasilisha mapungufu makubwa katika udhibiti wa ndani kwa wenye mamlaka za utawala na usimamizi. Lakini haitakuwa sahihi kuwasilisha mapungufu ya udhibiti wa ndani moja kwa moja kwa wasimamizi ikiwa mapungufu yanaweza kutilia shaka uadilifu au uwezo wa menejimenti. Kwa mfano, kunaweza kuwa na ushahidi wa ulaghai au kutofuata kwa makusudi sheria na kanuni za menejimenti, au menejimenti inaweza kuonesha kutokuwa na uwezo wa kusimamia utayarishaji wa taarifa za fedha jambo ambalo linaweza kutilia shaka uwezo wa menejimenti. [28]

Wakaguzi wengi wa ndani huwasilisha kasoro kama hizo kwa kamati ya ukaguzi (safu ya kazi ya kutolea taarifa) na si kwa kamati ya fedha ya halmashauri. Mkaguzi mmoja wa ndani alieleza kuwa mapungufu hayo hayawezi kuripotiwa kwenye kamati ya fedha kwa sababu mkaguzi wa ndani anaripoti kiutawala kwa afisa mtendaji mkuu ambaye pia ni mkurugenzi mtendaji wa halmashauri na katibu wa kamati ya fedha. [29]

Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA) 260 (Vilivyorekebishwa) juu ya Mawasiliano na Wenye Dhamana ya Utawala vinabainisha kuwa, katika baadhi ya maeneo, mkaguzi anaweza kutakiwa na sheria au kanuni kuarifu chombo cha udhibiti au cha utekelezaji wa masuala ambayo yamewasilishwa kwa wenye mamlaka.[30]

Wakaguzi wa ndani waliohojiwa waligawanyika sawa kuhusu maoni iwapo kuna mahitaji ya kisheria au miongozo ya wao kuripoti wanapohisi kutofuatwa kwa sheria na kanuni au udanganyifu. Walizitaja mamlaka mbalimbali zitakazojulishwa kuwa ni Kamati ya Fedha ya Baraza la Madiwani, Sekretarieti ya Mkoa, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA), na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

26 Ofisi ya Waziri Mkuu– Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Halmashauri ya Mji wa Korogwe, Mkataba wa Huduma ya Ukaguzi wa Ndani, Uk. 7. Jambo la kufurahisha ni kwamba hati ya ukaguzi wa ndani, (sehemu ya 14) inasema kwamba inapaswa kupitishwa na mtendaji mkuu na baraza la madiwani.

27 ISA 260 (Revised), paragraph A7.

28 ISA 265, paragraphs 9, 10 and A20.

29 Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa, sehemu ya 7.

30 ISA 260 (Revised), paragraph A44.

Je, wanaopokea matokeo ya ukaguzi wanahakikisha kwamba yanazingatiwa ipasavyo?

Kufuatia Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA) 260 (Vilivyorekebishwa) kuhusu Mawasiliano na wenye dhamana ya Utawala, mkaguzi anapaswa kutathmini kama mchakato wa mawasiliano ya pande mbili kati ya mkaguzi na wenye dhamana ya utawala unaridhisha.[31] Wakaguzi wengi wa ndani waliohojiwa walikubali kuwa wajumbe wa kamati ya ukaguzi wanaweza kuelewa mambo yaliyotolewa na mkaguzi wa ndani, kwa mfano, kwa kuchunguza masuala na kuhoji mapendekezo, na pia wanafahamu jinsi masuala hayo yanavyoathiri majukumu yao.

Hata hivyo, ni nusu tu ya wakaguzi wa ndani wanaoamini kuwa wajumbe wa kamati ya fedha wanaweza kuelewa masuala ya ukaguzi na jinsi yanavyoathiri majukumu yao. Aidha, ni asilimia 50 tu ya wajumbe wa kamati za ukaguzi na asilimia 40 pekee ya wajumbe wa kamati za fedha ndio waliothibitisha kupokea taarifa na mafunzo ya jinsi masuala yanayojadiliwa na mkaguzi wa ndani yanavyoathiri majukumu yao. Wengi wa wajumbe wa kamati hiyo walisema kuwa mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri ndiye anayepaswa kuwajibika kutoa taarifa na mafunzo hayo.

3.5 Ufuatiliaji

Baada ya matokeo ya ushiriki wa ukaguzi kuripotiwa, mkaguzi wa ndani anatakiwa kufuatilia jinsi menejimenti inavyochukua hatua za kupunguza vihatarishi kwa kiwango kinachokubalika na taasisi.

Je, kazi ya ukaguzi wa ndani inafuatilia utekelezaji bora wa hatua za menejimenti?

Kiwango cha utendaji cha IPPF 2500 kinahitaji wakaguzi wa ndani kuanzisha mchakato wa ufuatiliaji ili kufuatilia na kuhakikisha kuwa hatua za usimamizi zimetekelezwa kwa ufanisi au kwamba menejimenti ya juu imekubali athari ya kutochukua hatua.

Wakaguzi wengi wa ndani waliohojiwa walieleza kuwa taratibu rasmi za ufuatiliaji zipo ili kufuatilia utekelezaji bora wa mapendekezo ya ukaguzi na maagizo ya wakaguzi wa ndani na nje, kamati ya ukaguzi na kamati ya fedha; baadhi ya wakaguzi wa ndani pia walivitaja vyombo vingine kuwa ni Mkaguzi Mkuu wa Ndani, Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma, na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa.

Mmoja wa wakaguzi wa ndani alionesha wasiwasi wake kwamba mfumo wa sasa wa ufuatiliaji sio rafiki kwa watumiaji. IAGD ilieleza kuwa Mfumo wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi wa Serikali (GARI-ITS) unajumuisha mapendekezo na maelekezo kutoka kwa mkaguzi wa ndani na nje, Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali. Lakini changamoto za kiufundi na ukosefu wa mafunzo wa wadau vinakwamisha mchakato wa ufuatiliaji.

Je, kazi ya ukaguzi wa ndani inajadili hatari zinazokubaliwa na menejimenti na wenye dhamana ya utawala?

Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA) 265 kuhusu Kuwasilisha Mapungufu katika Udhibiti wa Ndani kwa wenye dhamana ya Utawala na Menejimenti vinaeleza kuwa pale ambapo hatua hazijachukuliwa kurekebisha upungufu mkubwa, mkaguzi anaweza kuiuliza menejimenti au wenye dhamana ya utawala ni kwa nini kuna mapungufu ambayo hayajarekebishwa. Kushindwa kuchukua hatua na ama kukosekana kwa maelezo yenye mantiki, pia ni sehemu ya upungufu mkubwa.

Wajumbe wote wa kamati za ukaguzi walithibitisha wakati wa mahojiano kwamba wakaguzi wa ndani wanauliza menejimenti kwa nini mapendekezo na maagizo ya ukaguzi yaliyowasilishwa hapo awali hayajatekelezwa, na wakaguzi wote wa ndani walithibitisha kuwa menejimenti inatoa maelezo yenye mantiki kwanini hayajatekelezwa.[32] Hata hivyo, uchambuzi wa ripoti za ukaguzi wa ndani unaibua maswali kuhusu uhalali wa majibu haya ya usaili. Ripoti moja ya ukaguzi wa ndani inatarajia menejimenti ya LGA "kujenga tabia ya kujibu kikamilifu" masuala yaliyojitokeza kwa kuzingatia mapendekezo yote yaliyotolewa na wakaguzi. Kwa hivyo, majibu ya masuala hadi sasa bado yanasubiriwa. Ripoti nyingine iliyochambuliwa ya ukaguzi wa ndani inapendekeza usimamizi wa halmashauri "kuweka juhudi zaidi ili kukamilisha utekelezaji wa hoja zilizosalia." Mifano hii miwili inaonesha kwamba wakaguzi wa ndani hawawezi kila wakati kutilia maanani maelezo ya kimantiki ya menejimenti, wanapofuatilia utekelezaji wa mapendekezo na maagizo ya ukaguzi yaliyowasilishwa hapo awali.

31 ISA 260 (Revised), paragraphs 22 and A51.

32 Ikumbukwe kwamba hati ya ukaguzi wa ndani ya Halmashauri ya Jiji la Mbeya (Uk 7) inahitaji majibu ya menejimenti kujumuisha ratiba ya hatua zinazotarajiwa kuchukuliwa na maelezo ya mapendekezo ambayo hayajashughulikiwa.

Kiwango cha IPPF 2600 kinasema iwapo mkaguzi wa ndani atahitimisha kuwa menejimenti imekubali kiwango cha hatari ambacho kinaweza kisikubalike kwa taasisi, mkaguzi wa ndani lazima ajadili suala hilo na menejimenti ya juu. Iwapo mkaguzi wa ndani atabaini kuwa suala hilo halijatatuliwa, mkaguzi wa ndani lazima awasilishe suala hilo kwa bodi. Ni nusu tu ya wakaguzi wa ndani waliohojiwa walisema kwamba waliwasilisha kesi kama hizo kwa kamati ya fedha ya baraza la madiwani. Mkaguzi mmoja wa ndani alibainisha kuwa menejimenti haielezi wazi iwapo imeamua kukubali baadhi ya vihatarishi. Wajumbe wengi wa kamati za fedha walikubali kwamba wana jukumu la kuamua ikiwa usimamizi umekubali vihatarishi ambavyo havikubaliki kwa taasisi. Pia walikubaliana kwamba wanaweza kuchukua hatua za kiutawala na kinidhamu dhidi ya watu binafsi, na wanaweza pia kuchukua matokeo ya kitaasisi. Mjumbe mmoja alieleza kuwa kamati ya fedha itaandaa kikao bila mkurugenzi mtendaji wa halmashauri na kutoa taarifa kwa Sekretarieti ya Mkoa na TAMISEMI kwa hatua zaidi. Wajumbe wote wa kamati ya fedha walithibitisha kuwa tathmini ya utendaji kazi wa Afisa Masuuli inahusishwa na kusimamia utekelezaji bora wa mapendekezo na maagizo ya ukaguzi.

4 Mjadala

4.1 Kuongeza Thamani

Shughuli ya ukaguzi wa ndani huongeza thamani katika mfumo wa usimamizi wa fedha za umma nchini kwa vile zinazingatia malengo ya taasisi na matarajio ya menejimenti. Pia zinatoa huduma za ushauri ili kuimarisha utawala, udhibiti wa vihatarishi na wadau katika ngazi ya serikali za mitaa na serikali kuu. Hata hivyo, thamani zaidi inaweza kuongezwa kwa kuzingatia mazingira ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kama vile hali mbaya ya ufadhili au udhaifu wa udhibiti, mambo ambayo yanaweza kuwa sababu kuu ya menejimenti ya Halmashauri kutozingatia udhibiti wa ndani.

Wigo wa Kazi za Mkaguzi wa ndani ni mpana

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa kazi ya ukaguzi wa ndani huongeza thamani kwa taasisi na wadau wake wote. Usaidizi wa jumla kutoka kwa wadau wote ni muhimu kwani mafanikio ya mageuzi ya usimamizi wa fedha za umma si tu suala la kiufundi bali pia ni suala la uchumi wa kisiasa.

Maoni ya kawaida ni kwamba 'uzingatiaji na taratibu za kifedha' na 'utendaji bora' vyote ni vipaumbele vya usimamizi wa fedha za umma kuliko kuhakikisha kuna 'nidhamu ya fedha' pekee. Matokeo haya yanaonesha kuwa wigo wa kazi ya ukaguzi wa ndani ni mpana na unakuza matumizi bora na ya ufanisi ya rasilimali.

IAGD na wakaguzi wa ndani wana maoni yanayofanana kwa kiasi kikubwa kuhusu maeneo yenye vihatarishi ya vipaumbele vya sasa (linganisha Jedwali 3) na pande zote mbili zilikubali kwamba kuelekeza nguvu kwenye rasilimali za ukaguzi wa ndani kwenye 'usimamizi wa mali' kungepandisha thamani juu zaidi. Lakini kuelekeza upya shughuli ya ukaguzi kwenye maeneo hatarishi ni vigumu ikiwa kiwango kilichopo cha utumishi na utaalamu hakitoshi. Wazo la kuunda timu maalum za serikali kuu kufanya ukaguzi maalum limekataliwa na IAGD na wakaguzi wa ndani. Miongozo inaruhusu utumaji wa wataalam wengine ikiwa hakuna afisa aliye na ujuzi unaohitajika; hata hivyo, hili linaweza lisifae kwa Halmashauri nyingi zisizo na fedha.

Kazi ya ukaguzi wa ndani inazingatia maoni kutoka kwa menejimenti ya juu

Wengi, ingawa si wote, wakaguzi wa ndani huzingatia vipaumbele vya kimkakati kupitia michango kutoka mamlaka nyingine kama vile Mkaguzi Mkuu wa Ndani na Mdhibiti na CAG, na kwa kawaida michango hii inaendana na tathmini ya vihahatarishi vya Halmashauri. Uthabiti huu ni muhimu ili kuhakikisha kuwa Halmashauri zinathamini matokeo ya ushiriki wa ukaguzi na kuhakikisha ufuatiliaji wenye ufanisi. Ili kulinda umiliki na uhuru wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa, wakaguzi wa ndani wanapaswa kuwa na mamlaka ya kuzingatia, na ikiwezekana kukataa, maombi kutoka kwa mamlaka ya serikali kuu ambayo hayaendani na tathmini ya vihahatarishi iliyoandikwa na Halmashauri.

Huduma za ushauri huimarisha utawala, udhibiti wa vihatarishi na michakato ya udhibiti

Wakaguzi wote wa ndani wana mamlaka makubwa na wanatoa huduma za ushauri kwa wateja mbalimbali katika ngazi ya serikali za mitaa na serikali kuu. Ni muhimu pia wakaguzi wa ndani kuzingatia maoni ya kimkakati kutoka kwa Kamati ya Uongozi ya Pamoja ya Mpango wa Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma na Kamati ya Utekelezaji ya Programu ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ili kuhakikisha kuwa watunga sera katika ngazi ya serikali kuu wanapata uelewa wa kutosha kuhusu mazingira halisi ya ndani.

Huduma za uhakiki hazizingatii sababu zote za msingi

Ripoti za ukaguzi wa ndani zinapaswa kuwa na matokeo ya tathmini sawia, ya ukweli, sahihi na inayozingatia mazingira yote muhimu. Hata hivyo, wakaguzi wa ndani na wajumbe wa kamati za ukaguzi wanaonekana kutofahamu mazingira ambapo watendaji wa serikali kuu wanakuwa ndio chanzo kwa menejimenti ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kutozingatia udhibiti wa ndani.

Katika mfumo wa serikali ya Tanzania wa ugatuzi wa madaraka, Mamlaka za Serikali za Mitaa zina jukumu la kufikisha bidhaa na huduma za umma kwa wananchi, wakati serikali kuu ina jukumu la kudhibiti na kufadhili bidhaa na huduma hizo. Utegemezi huu unaweza kuleta uzingatiaji dhaifu au utendaji kazi duni katika ngazi ya serikali za mitaa, kutokana na maamuzi yanayofanywa kwenye ngazi ya serikali kuu. Kwa mfano, tathmini ya Matumizi ya Fedha za Umma na Uwajibikaji wa Kifedha wa Serikali za Mitaa (PEFA) 2016 iligundua kuwa mgawo wa fedha kutoka Hazina (ambapo fedha hazitolewi kama ilivyopangwa) ulisababisha baadhi ya Halmashauri kuweka ahadi za matumizi nje ya mfumo wa usimamizi wa kompyuta na kusababisha malimbikizo ya malipo.

Mwenendo huu unaweza kuelezewa na Hazina kwa kuweka kipaumbele katika nidhamu ya fedha na menejimenti ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka kipaumbele katika utoaji wa huduma bora kuliko ufuasi wa vigezo.[33] Mfano mwingine ni kwamba miongozo ya bajeti ya serikali kuu haizingatii hali ya usimamizi wa fedha za umma katika ngazi ya serikali za mitaa; wanazitaka Halmashauri kuandaa makadirio ya mapato na matumizi kwa miaka mitatu ijayo (Mfumo wa Matumizi ya Muda wa Kati (MTEF)) kwa mujibu wa Takwimu za Fedha za Serikali (GFS). Kwa minajili ya kuzingatia miongozo ya bajeti, Halmashauri huandaa makadirio ya miaka mitatu bila uchambuzi wowote wa kisayansi na kisha kutumia bajeti iliyoidhinishwa ya mwaka uliopita kama kikomo kwa mwaka wa fedha unaofuata. Matokeo yake, MTEF haiwezi kusaidia kikamilifu ugawaji wa rasilimali za kimkakati na bajeti ya utendaji.[34] Mifano hii miwili na ripoti ya mapitio ya muda wa kati ya Mpango wa Utawala Bora wa Kifedha wa kutathmini ubora wa ripoti za ukaguzi wa ndani zinaonesha kuwa utambuzi wa sababu za msingi (kama vile hali mbaya ya kifedha au ukiukwaji wa udhibiti) ni udhaifu. [35]

4.2 Mipango

Kazi ya ukaguzi wa ndani ina mipango kazi inayozingatia vihatarishi, lakini mapungufu ya rasilimali, uratibu dhaifu na ushirikiano wa shughuli ya ukaguzi wa nje huzuia ushughulikiaji bora wa ukaguzi na kusababisha kazi kurudiwa rudiwa.

Shughuli ya ukaguzi wa ndani hutumia mipango kazi inayozingatia vihatarishi

CAG alibainisha mwaka 2019 kuwa asilimia 30 ya Halmashauri 33 zilizokaguliwa hazina sera iliyoidhinishwa ya usimamizi wa vihatarishi, 81% hazikufanya tathmini ya vihatarishi, na 21% hazikutunza rejista za vihatarishi. Aidha, ripoti ya mapitio ya kipindi cha kati ya Mpango wa Utawala Bora wa Kifedha (2019) kuhusu ubora wa ripoti za ukaguzi wa ndani pia ilibaini kuwa Wizara, Idara na Wakala wa Serikali za Mitaa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizofanyiwa utafiti hazikufanya tathmini ya vihatarishi, au kulikuwa na uhusiano dhaifu kati ya hatari zilizoainishwa na mpango wa ukaguzi wa mwaka.[36] Aidha, ripoti ya mapitio ya kipindi cha kati ya Mpango wa Utawala Bora wa Kifedha (2019) kuhusu ubora wa ripoti za ukaguzi wa ndani pia ilibaini kuwa Wizara, Idara na Wakala na Serikali za Mitaa zilizofanyiwa tafiti nyingi hazikufanya tathmini ya vihatarishi au kulikuwa na uhusiano duni kati ya vihatarishi vilivyoainishwa na mpango wa ukaguzi wa mwaka.[37]

Tofauti na tathmini hizi za mwaka 2019, wakaguzi wa ndani wa Mamlaka za Serikali za Mitaa na wajumbe wa kamati za ukaguzi walieleza wakati wa mahojiano kuwa mipango ya ukaguzi wa ndani inategemea rejista za vihatarishi na kwamba waratibu wa viashiria hatarishi wanawajibishwa. Walitoa wito wa ufadhili zaidi kwa shughuli za udhibiti wa vihatarishi na mafunzo ya kina zaidi yanayolingana na wajibu na majukumu ya waratibu wa vihatarishi.

Mkakati una dhima ya kupachika Udhibiti wa Vihatarishi vya Biashara (ERM) katika taasisi zote za utumishi wa umma, na unatoa mpango wa utekelezaji wa kina ili kuimarisha uhakiki wa ubora wa udhibiti wa vihatarishi na kujenga uwezo, kupitia muundo wake wa utawala, na kuunganisha uzoefu wa udhibiti wa vihatarishi katika mchakato wa bajeti. Moja ya kazi muhimu itakuwa ni kuhakikisha kuwa vitengo vya udhibiti wa vihatarishi vinapatiwa fedha za kutosha na mafunzo ya kina zaidi.

Shughuli ya ukaguzi wa ndani haina rasilimali za kutosha

Mwaka 2019, CAG aligundua kuwa asilimia 86 ya vitengo vya ukaguzi wa ndani vya Halmashauri vilivyokaguliwa havina rasilimali za kutosha na hazina fedha, kompyuta au vifaa vingine. Matokeo ya utafiti yanathibitisha tathmini hii na kukadiria uhaba wa fedha wa kazi ya ukaguzi wa ndani kwa takriban 40% -50%, na kusababisha ucheleweshaji au wigo finyu wa ukaguzi. Pengo hili kubwa la ufadhili linaweza kufafanuliwa kwa sababu mbili: kwanza, wigo uliopanuliwa wa kazi ya ukaguzi wa ndani ambayo inajumuisha sio tu mapitio ya miamala ya kifedha na taarifa lakini pia uchunguzi wa aina kubwa za mifumo ya udhibiti; sababu ya pili inaweza kuwa mchakato wa nyongeza wa bajeti ambao kwa kiasi kikubwa unategemea bajeti ya mwaka uliopita kwa kuzingatia aina finyu ya ongezeko au kupungua. Kwa asili yake, ongezeko la bajeti haliwezi kukidhi mabadiliko ya kipekee katika wigo wa kazi ya ukaguzi wa ndani na mzigo mkubwa wa kazi zinazoendana.

33 PriceWaterhouseCoopers (2016), Consolidated Sub-National Government PEFA Assessment report, p. 79.

34 PriceWaterhouseCoopers (2016), Consolidated Sub-National Government PEFA Assessment report, p. 60.

35 Good Financial Governance Programme (2019), Compliance Verification of Internal Audit Reports of Selected Institutions in the Tanzanian Public Sector, Mid-Term Review Report, p. 29.

36 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (2019), Ripoti Kuu ya Mwaka ya Ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mtaa (LGAs) kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, kiambatanisho 27.

37 Good Financial Governance Programme (2019), Compliance Verification of Internal Audit Reports of Selected Institutions in the Tanzanian Public Sector, Mid-Term Review Report, p. 6.

Mkakati unakiri kuwa vitengo vya ukaguzi wa ndani na kamati za ukaguzi hazina mgao wa bajeti unaotosheleza hivyo kudhoofisha uhuru wao kama taasisi. Kuna haja ya kuwa na mjadala wa jinsi ambavyo pengo kati ya wigo mpana na vikwazo vinavyoenea vya rasilimali linapaswa kupunguzwa. Uamuzi huo unaweza kuachwa kwa Halmashauri husika, au inawezekana kufikiria kuweka kiwango kikubwa ambacho kinafadhiliwa na serikali kuu. Mbinu hii ya mwisho, hata hivyo, itadhoofisha umiliki wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wa shughuli ya ukaguzi wa ndani.

Kukosekana kwa uhuru huzuia uratibu na ushirikiano na shughuli ya ukaguzi wa nje

Tathmini ya IAGD na Mpango wa Utawala Bora wa Fedha (2018) ulitaja kuwa uhusiano kati ya wakaguzi wa nje na wa ndani una sifa ya kutoaminiana. [38] Wakati wa mahojiano, wakaguzi wengi wa ndani walidai kuthibitisha uhuru wao wa taasisi kwa kamati ya fedha. Lakini mtazamo huu unakinzana na ukweli kwamba mkaguzi wa ndani anaripoti kiutendaji kwa kamati ya ukaguzi, ambayo si chombo cha usimamizi cha Halmashauri. Kamati ya ukaguzi inamshauri mtendaji mkuu/mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri pekee anayemwakilisha mkaguliwa. Tathmini ya IAGD na Mpango wa Utawala Bora wa Kifedha (2018) pia inasisitiza kwamba "kwa kuzingatia muundo wa sasa wa kisheria, kamati za ukaguzi haziwezi kutimiza jukumu lao kama chombo huru cha ushauri na usimamizi." [39]

Hii inamaanisha kwamba kuna makubaliano kati ya wadau kuwa uhusiano wa kiutendaji wa kuripoti kwa kamati ya ukaguzi unadhoofisha uhuru wa mkaguzi wa ndani; hii inaweza kuelezea kutoaminiana kwa wakaguzi wa nje na kuzuia uratibu na ushirikiano wenye ufanisi kwa shughuli ya ukaguzi wa ndani.

4.3 Ushiriki katika Ukaguzi

Kazi ya ukaguzi wa ndani inategemea uhakiki wa ubora wa ndani na nje na inapata ushauri na usaidizi stahili ili kuendana na viwango vya kimataifa, lakini shughuli za dharura na programu za maendeleo ya wafanyakazi zinakandamiza mapato na vyanzo vya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Shughuli ya ukaguzi wa ndani hupata ushauri na usaidizi mwafaka ili kuendana na viwango vya kimataifa

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa wakaguzi wengi wa ndani wanatumia Kitabu cha Ukaguzi wa Ndani na Kitabu cha Msaada cha Ukaguzi wa Ndani kilichotolewa na Mkaguzi Mkuu wa Ndani, na wanaweka wazi kutokidhi vigezo vya IPPF pamoja na mipango ya utekelezaji kwa kamati za ukaguzi na kamati ya fedha. Hata hivyo, majibu haya kwa kiasi fulani yanapingana na ripoti ya mapitio ya katikati ya muhula ya Programu ya Utawala Bora wa Kifedha (2019) kuhusu ubora wa ripoti za ukaguzi wa ndani, ambayo ilibaini kuwa ripoti nyingi za mwaka hazioneshi kama kitengo cha ukaguzi wa ndani kilizingatia vigezo vya IPPF; kwa upande mwingine, ripoti haioneshi kama uchunguzi unahusu MDAs au LGAs. Uchunguzi zaidi unaweza kufichua iwapo vielezo vya kuripoti vinahitaji kufichua kutofuatana kwa IPPF na ikiwa baadhi ya wakaguzi wa ndani ama hawafuati kanuni zao au kama wana wasiwasi wa kuripoti.

Uhaba wa rasilimali na shughuli za dharura huzuia kufikiwa kwa malengo ya ukaguzi

Matokeo ya utafiti yanathibitisha ripoti na tafiti za awali zinazoonesha kuwa uhaba wa rasilimali umeenea. Katika mazingira duni kama haya, shughuli za ziada za dharura huleta changamoto kubwa katika kufikiwa kwa malengo ya ukaguzi kwani si mara zote bajeti hurekebishwa kulingana na mzigo wa kazi ulioongezeka.

Katika mazingira yenye fursa kidogo au pasipo na fedha, mpango wa ukaguzi lazima uwe rahisi kubadilika ili kushughulikia dharura. Zaidi ya hayo, ripoti ya mapitio ya katikati ya muhula ya Programu ya Utawala Bora wa Fedha (2019) kuhusu ubora wa ripoti za ukaguzi wa ndani pia inapendekeza kwamba matokeo ya ukaguzi wa dharura yanapaswa kuripotiwa kama yalivyo, na si kama shughuli za ushauri kwa kuzingatia viwango vya Taasisi ya Wakaguzi wa Ndani. [40]

38 Good Financial Governance Programme (2018), Strategy for the further development of the Internal Audit System of the Public Sector of Tanzania, Phase I: Stock Taking and Assessment and Phase II: Root Cause Analysis, p. 30.

39 Good Financial Governance Programme (2018), Strategy for the further development of the Internal Audit System of the Public Sector of Tanzania, Phase I: Stock Taking and Assessment and Phase II: Root Cause Analysis, p. 29.

40 Good Financial Governance Programme (2019), Compliance Verification of Internal Audit Reports of Selected Institutions in the Tanzanian Public Sector, Mid-Term Review Report, p. 60.

Uhakiki wa ubora unajumuisha tathmini za ndani na nje

Ripoti ya mapitio ya kipindi cha kati ya Programu ya Utawala Bora wa Fedha (2019) kuhusu ubora wa ripoti za ukaguzi wa ndani ilibainisha kuwa waliofanyiwa majaribio ya awali walikuwa bado hawajaanza kutumia Zana ya Ufuatiliaji. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa Zana hii ni muhimu sana katika kusaidia ufuatiliaji wa ndani na usimamizi unaoendelea wa shughuli za ukaguzi wa ndani. Lakini changamoto za mawasiliano katika uhakiki wa ubora na uboreshaji wa matokeo kwa IAGD yanaweza kukwamisha uratibu na uwezeshaji wa mipango ya kurekebisha ina yofanywa na serikali kuu.

Programu za maendeleo ya wafanyakazi zinakwamishwa na uhaba wa fedha

Licha ya jitihada za mamlaka za serikali za mitaa na serikali kuu kushughulikia mahitaji yaliyopo ya mafunzo, wakaguzi wa ndani wana wasiwasi kuwa programu za maendeleo ya wafanyakazi zinakwamishwa na uhaba wa fedha. Kwa mujibu wa kifungu cha 38 cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2010, IAGD ina jukumu la kuwezesha maendeleo ya kada ya ukaguzi kupitia upangaji wa bajeti, mapitio na tathmini, pamoja na kuandaa ripoti za kitaalamu zinaonesha jitihada za kuleta maendeleo.

Upangaji jumuishi, ufuatiliaji na tathmini ya mipango ya maendeleo ya wafanyakazi katika ngazi ya serikali ya mitaa na serikali kuu ungesaidia kuratibu juhudi zote za mafunzo na kuhakikisha kwamba ujuzi na utaalamu wa kada ya ukaguzi wa ndani unalingana na maeneo ya vihatarishi yaliyopewa kipaumbele.

4.4 Utoaji Taarifa

Kukosekana kwa mawasiliano kwa wakati kati ya wakaguzi wa ndani wa Mamlaka za Serikali za Mitaa na mamlaka za serikali kuu kunazuia uzingatiaji wa matokeo ya ukaguzi. Zaidi ya hayo, uwepo wa menejimenti wakati wa mikutano na kamati ya fedha unaweza kukatisha tamaa wakaguzi wa ndani kuripoti mapungufu makubwa ambayo yanaweza kutilia shaka uadilifu au uwezo wa menejimenti.

Mawasiliano ya matokeo ya ukaguzi yanacheleweshwa na matatizo ya utekelezaji wa bajeti

Ripoti ya mapitio ya kipindi cha kati ya Programu ya Utawala Bora wa Fedha (2019) kuhusu ubora wa ripoti za ukaguzi wa ndani ilibaini kuwa ucheleweshaji wa utoaji wa ripoti za ukaguzi ulisababishwa na majibu ya menejimenti kuchelewa na pia kuchelewa kwa majibu ya vikao vya kamati ya ukaguzi. [41] Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa ucheleweshaji pia unasababishwa na matatizo ya utekelezaji wa bajeti ambayo huathiri utekelezaji wa shughuli za ukaguzi wa ndani.

Utoaji wa muhtasari wa ripoti unatatizwa na wadau wanaochelewesha majibu

Tathmini Ndogo ya Kitaifa ya Matumizi ya Umma na Uwajibikaji wa Fedha (PEFA) (2016) ilionesha kuwa ripoti za ukaguzi wa ndani hazipelekwi kwa wakati kwa mamlaka za nje - ikiwa ni pamoja na CAG, IAG, na OR-TAMISEMI au RS. [42] Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa wakaguzi wa ndani wa Mamlaka za Serikali za Mitaa huwasilisha ripoti kwa kuchelewa na si mara zote zinakidhi viwango na muundo uliowekwa. Changamoto nyingine ya utayarishaji wa muhtasari wa ripoti ni kucheleweshwa majibu kutoka kwa mamlaka za serikali kuu. Kuchelewesha majibu kutoka kwa wadau katika ngazi ya serikali za mitaa na serikali kuu kunaweza kueleza kwa kiasi fulani kwa nini IGAD haitoi mrejesho wa kutosha kwa wakaguzi wa ndani kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Umma ya 2010.

Kitengo cha ukaguzi wa ndani hakiwasilishi matokeo ya ukaguzi kwa wahusika

Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa (2009), kifungu cha 13, inabainisha kuwa mkaguzi wa ndani anaripoti kiutawala kwa mtendaji mkuu, wakati ngazi ya utendaji ni kwa kamati ya ukaguzi (kifungu cha 12). Tathmini ndogo ya Kitaifa ya PEFA (2016) ilibainisha kuwa lengo la vikao vya kamati ya ukaguzi lilikuwa ni kuidhinisha maamuzi badala ya kuchunguza na kuishauri menejimenti ya halmashauri. [43]

41 Good Financial Governance Programme (2019), Compliance Verification of Internal Audit Reports of Selected Institutions in the Tanzanian Public Sector, Mid-Term Review Report, p. 8.

42 PriceWaterhouseCoopers (2016), Consolidated Sub-National Government PEFA Assessment report, p. 85.

43 PriceWaterhouseCoopers (2016), Consolidated Sub-National Government PEFA Assessment report, p. 82.

Mkakati unakiri kwamba kamati ya ukaguzi inatoa ushauri kwa mtendaji mkuu pekee na hivyo si chombo cha uangalizi. Kwa sababu hiyo, iliweka lengo la kuanzisha 'kamati ya uangaliza wa ukaguzi' katika taasisi zote za utumishi wa umma.

Lakini Halmashauri tayari zina chombo cha uangalizi chenye jukumu la kudhibiti na kusimamia fedha za Halmashauri: baraza la madiwani na kamati yake ya fedha. Kama ilivyobainishwa awali, kupitishwa kwa viwango vya IPPF na dhana ya kisasa ya kazi ya ukaguzi wa ndani, inahitaji kubadilisha hali ya taasisi ya wakaguzi wa ndani na wigo kutoka mfumo wa "ukaguzi kwa menejimenti" hadi "ukaguzi wa menejimenti". Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa mabadiliko ya uhusiano wa mamlaka hayaungwi mkono na wajumbe wa kamati za ukaguzi, ambao wana wasiwasi kuwa uhusiano wa utendaji kati ya mkaguzi wa ndani na kamati ya fedha unaweza kusababisha kutoelewana.

Wakaguzi wa ndani hawakutani na kamati ya fedha bila uwepo wa menejimenti

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa wadau wengi wa serikali za mitaa wanaridhishwa na ukweli kwamba mkaguzi wa ndani hakutani na kamati ya fedha ya halmashauri bila menejimenti kuwepo. Kwa upande mwingine, wanaunga mkono kikao cha mkaguzi wa ndani na kamati ya ukaguzi bila menejimenti kuwepo.

Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa (2009) inawataka wajumbe wawili wa kamati ya ukaguzi kuteuliwa kutoka nje ya halmashauri. [44] Hata hivyo, wajumbe wa kamati ya ukaguzi wanafanya kazi ya ushauri tu, huku usimamizi wa Halmashauri unafanywa na kamati ya fedha ya halmashauri. Kukutana na kamati ya fedha na uwepo wa menejimenti kunaweza kuathiri uhuru wa mkaguzi wa ndani, kutokuwa mkweli kwani mkaguzi wa ndani anaripoti kiutawala kwa mtendaji mkuu, anayemwakilisha mkaguliwa.

Mapungufu makubwa katika udhibiti wa ndani hayajawasilishwa kwa ngazi husika ya menejimenti

Wakaguzi wa ndani hawaripoti mapungufu makubwa ambayo yanaweza kutilia shaka uadilifu (kama vile kutofuata kwa makusudi sheria na kanuni au udanganyifu) au uwezo wa menejiment (kama vile kutokuwa na uwezo wa kusimamia utayarishaji wa kuridhisha wa taarifa za fedha) kwa kamati ya fedha ya halmashauri kwa sababu mtendaji mkuu pia ni mkurugenzi mtendaji wa halmashauri na katibu wa kamati ya fedha. Kwa sababu hiyo, wakaguzi wa ndani huripoti mapungufu makubwa kwa kamati ya ukaguzi, ambayo hufanya kazi ya ushauri lakini sio kazi ya uangalizi.

Mkakati huu ulitayarisha dira ya "kuanzisha kamati huru na zenye ufanisi za ukaguzi katika sekta ya umma ya Tanzania kupitia sheria kuu". [45] Ili kufikia uzingatiaji wa viwango vya kimataifa vya ukaguzi wa hesabu, swali ni iwapo, 'kamati za uangalizi wa ukaguzi' zilizoanzishwa hivi karibuni zitawajibika kwa utawala, na jinsi majukumu yao yatakavyolinganishwa na kamati za fedha za halmashauri zilizopo, ambazo zina jukumu la "kudhibiti na kusimamia". fedha za Halmashauri". [46]

Wajumbe wa kamati ya fedha wanahitaji taarifa na mafunzo zaidi

Mkakati uliweka lengo la kuzifanya kamati zote za ukaguzi kuwa huru na zenye ufanisi. Ingawa wajumbe wa kamati ya ukaguzi wanaonekana kuwa na uwezo wa kuelewa masuala ya ukaguzi na jinsi yanavyoathiri majukumu yao, wajumbe wa kamati ya fedha wanahitaji taarifa zaidi na mafunzo ili kutekeleza wajibu wao wa kudhibiti na kusimamia fedha za halmashauri. Kwa vile Halmashauri nyingi hazina nyenzo na utaalamu wa kutosha wa kutoa semina na mafunzo kwa wafanyakazi na viongozi wao, mjadala unaweza kuwa jinsi gani Ofisi ya Rais TAMISEMI na IAGD watahakikisha kuwa kamati za fedha zinawezeshwa ipasavyo kutekeleza majukumu na wajibu wao kwa ufanisi. [47]

4.5 Ufuatiliaji

Kuna mchakato rasmi wa ufuatiliaji wa mapendekezo ya ukaguzi, lakini majibu yasiyoeleweka ya menejimenti yanaweza kuzuia udhibiti wa vihatarishi ambavyo havikubaliki kwa taasisi.

44 Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa (2009), Sehemu ya 12.

45 Ministry of Finance and Planning and Good Financial Governance Programme (2019), Strategy for the Further Development of the Internal Audit System in the Public Sector of Tanzania, p. 10.

46 Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa (2009), sehemu ya 6.

47 Ikumbukwe kwamba mwaka 2019, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na IAGD walikubali pendekezo la CAG kwamba "wataendelea kuhakikisha kuwa kamati za ukaguzi wa ndani zinawezeshwa ipasavyo kutimiza majukumu yao kwa ufanisi." Linganisha na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (2019), Ripoti Kuu ya Mwaka ya Ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, Uk. 277.

Kufuatilia utekelezaji kwa ufanisi wa hatua za manejimenti kunahitaji msaada wa kitaalam

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa kuna utaratibu rasmi wa ufuatiliaji katika ngazi ya serikali za mitaa, lakini ufuatiliaji wa mapendekezo ya ukaguzi katika ngazi ya serikali kuu bado unakabiliwa na changamoto za kiufundi. Ili kutatua suala hili, Mkakati unajumuisha shughuli ya "kuboresha zana iliyopo ya ufuatiliaji wa mapendekezo ya ukaguzi (GARI-ITS) ili kufuatilia kufungwa kwa mapendekezo ya ukaguzi na kufanyakazi katika Wizara, Idara, Idara na Wakala wa Serikali, RSs na Halmashauri.

Vihatarishi vinavyokubaliwa na menejimenti vinaweza visikubalike kwa taasisi

Uchambuzi wa ripoti za ukaguzi wa ndani unaonesha kuwa baadhi ya wakaguzi wa ndani wanatarajia menejimenti kuzingatia "mapendekezo yote yaliyotolewa na wakaguzi". Ingawa majibu duni ya usimamizi kwa mapendekezo ya ukaguzi ni tatizo linalojulikana sana, itakuwa ni makosa kudhani kwamba mapendekezo yote ya ukaguzi yanapaswa kutekelezwa licha ya kuwa na sababu za msingi za kutofanya hivyo. [48]

Huwa inatokea, ambapo menejiment imeamua kukubali vihatarishi fulani ambavyo havikubaliki kwa taasisi. Wakaguzi wa ndani wanapaswa kuwasilisha kesi kama hizo kwa kamati ya fedha ya halmashauri, ambayo ina jukumu la kudhibiti na kusimamia fedha za Halmashauri.

Hata hivyo, ripoti ya mapitio ya kati ya muhula ya Programu ya Utawala Bora wa Fedha (2019) kuhusu ubora wa ripoti za ukaguzi wa ndani ilibaini kuwa ripoti za ukaguzi wa ndani za wajaribiwa wote hazikujumuisha uchambuzi wa tathmini ya vihatarishi, mapendekezo ambayo yaliripotiwa kutekelezwa, yametekelezwa kwa kiasi, au hayajatekelezwa. [49]

48 Mathalan, utekelezaji wa hatua za ziada za udhibiti unaweza kuhitaji kuajiri wafanyakazi wa ziada kunapokuwa na bajeti ndogo kwa ajili ya rasilimali watu.

49 Good Financial Governance Programme (2019), Compliance Verification of Internal Audit Reports of Selected Institutions in the Tanzanian Public Sector, Mid-Term Review Report, p. 54.

5 Hitimisho

Mafanikio ya malengo ya maendeleo ya Tanzania yanategemea kazi thabiti ya ukaguzi wa ndani ambayo inaimarisha utawala, usimamizi wa vihatarishi na udhibiti ili kupunguza makosa ya utunzaji wa kumbukumbu, ubadhirifu wa mali na upotevu wa rasilimali. Mfumo wa Kimataifa wa Uzoefu wa Kitaaluma (IPPF) uliidhinishwa na Bodi ya Kitaifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu mwaka 2017. Unajumuisha ufafanuzi wa ukaguzi wa ndani, Kanuni za lazima za Maadili pamoja na Sifa na Viwango vya Utendaji vinavyotumika kwa huduma zote za ukaguzi wa ndani katika nchi.

Ili kuhakikisha uhuru na usawa kwa wakaguzi wa ndani, viwango hivi vinahitaji kubadilisha hali na wigo wa taasisi kutoka kwenye utaratibu wa awali wa "ukaguzi kwa mnejimenti" na kuwa wa kisasa wa "ukaguzi wa menejimenti". Upangaji upya wa kimkakati kama huo ni changamoto kubwa, lakini IPPF inatoa mwongozo wa wazi, jinsi mambo yanavyopaswa kubadilika. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa wigo wa kazi ya ukaguzi wa ndani ni mpana: unatoa huduma za uhakiki na ushauri kwa wateja katika ngazi ya serikali za mitaa na serikali kuu ili kuimarisha utawala, usimamizi wa vihatarishi, na mifumo mbalimbali ya udhibiti. Hata hivyo, wigo huo unabanwa na mapungufu ya rasilimali: kazi ya ukaguzi wa ndani haina fedha na wakaguzi wa ndani mahiri wa kutosha kukamilisha shughuli zilizopangwa na uwepo wa shughuli za dharura, kwa wakati.

Changamoto nyingine ni ukosefu wa uhuru wa ukaguzi wa ndani: wakaguzi wa ndani wanaripoti kiutendaji kwa kamati ya ukaguzi ambayo zaidi inaundwa na wasimamizi wakuu wanaomshauri mtendaji mkuu ambaye anamwakilisha mkaguliwa. Hii inamaanisha kuwa mfumo bado unafuata mfumo wa zamani wa "ukaguzi kwa umenejimenti". Kutokana na hali hiyo, wakaguzi wa ndani wanasita kuripoti mapungufu makubwa ambayo yanaweza kutilia shaka uadilifu au uwezo wa menejimenti kwa kamati ya fedha ya halmashauri, ambayo ina jukumu la kudhibiti na kusimamia fedha za Halmashauri. Ukosefu wa uhuru pia unazuia uratibu na ushirikiano na kazi ya ukaguzi wa nje ili kuhakikisha ukaguzi wa kutosha na kuzuia kurudiwa kwa shughuli.

Nje ya changamoto hizi za kimuundo za kufuata viwango vya kimataifa vya ukaguzi wa ndani, utafiti pia ulibainisha masuala ya uchumi wa kisiasa na muktadha wa mageuzi ambayo yanaweza kuathiri maendeleo ya mfumo wa ukaguzi wa ndani katika sekta ya umma. Kwanza, wajumbe waliohojiwa wa kamati ya ukaguzi hawakuunga mkono wazo la kuanzisha uhusiano wa kiutendaji wa taarifa kati ya mkaguzi wa ndani na kamati ya fedha ya halmashauri. Pili, katika mfumo wa ugatuaji wa madaraka, uundaji na ufadhili wa programu za maendeleo ya watumishi unahitaji kuratibiwa vyema kati ya mamlaka kuu na serikali za mitaa ili kuhakikisha kwamba ujuzi na utaalamu wa kada ya ukaguzi wa ndani unalingana na maeneo vipaumbele ya vihatarishi vya Halmashauri. Tatu, kwa kuwa shughuli nyingi za ndani zinagharamiwa na kudhibitiwa na mamlaka mbalimbali za serikali kuu, mawasiliano kati ya wakaguzi wa ndani wa Mamlaka za Serikali za Mitaa na mamlaka za serikali kuu yanahitaji kuimarishwa ili kuhakikisha kuwa matokeo ya ukaguzi yanazingatiwa ipasavyo.

6 Mapendekezo

Mapendekezo yafuatayo yanaweza kuchangia mchakato wa kina na wa muda mrefu wa mazungumzo ya wadau kuhusu maendeleo ya mfumo wa ukaguzi wa ndani ili kuendana na viwango vya kimataifa vya ukaguzi wa ndani.

Kuongeza thamani kwa kuboresha uratibu kati ya mamlaka za serikali za mitaa na serikali kuu

- Kazi ya ukaguzi wa ndani haina wafanyakazi wa kutosha, ujuzi au utaalamu katika maeneo mbalimbali yenye vihatarishi. Mjadala unaweza kuwa ni jinsi gani shughuli za ukaguzi wa ndani zinaweza kufanywa na wataalam wengine wa nje kwa kuzingatia vyanzo vichache vya mapato vya Mamlaka za Serikali za Mitaa
- Mratibu wa usimamizi wa vihatarishi wa Halmashauri anaweza kushauri kama mchango wa serikali kuu katika mchakato wa kupanga ni kipaumbele cha Halmashauri kwa kuzingatia tathmini yake iliyoandikwa ya vihatarishi.
- Wakaguzi wa ndani wanahitaji mafunzo zaidi juu ya kufanya uchambuzi wa vyanzo. Ikiwa sababu ya msingi ni mhusika katika ngazi ya serikali kuu, mkaguzi wa ndani anapaswa kushughulikia upande uhusika ambao unawajibika kwa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kupitia IAGD.

Kuimarisha mchakato wa kupanga ili kuhakikisha kuwa mipango ya ukaguzi wa ndani ina rasilimali za kutosha na inaratibiwa na Ofisi za ukaguzi wa nje

- Kitengo cha usimamizi wa vihatarishi kinaweza kupewa ufadhili wa kutosha na mafunzo ya kina zaidi.
- Wakaguzi wa ndani na bodi ya uangalizi ya Halmashauri wanapaswa kuhakikisha kuwa wigo wa mpango kazi wa ukaguzi wa ndani unawiana na rasilimali zilizopo.
- Wakaguzi wa ndani wanapaswa kuripoti kiutendaji kwa bodi ya uangalizi ya Halmashauri ili kuhakikisha uhuru wao kama taasisi na uaminifu wa kazi ya ukaguzi wa nje.

Kuimarisha mchakato wa ushiriki wa ukaguzi ili kushughulikia dharura na kuhakikisha ustadi wa wakaguzi wa ndani na huduma wanazotoa

- IPPF inaweza kuwa sehemu ya mtaala wa wahasibu, wakati wakaguzi wa ndani wanapaswa kupata mafunzo endelevu kuhusu mabadiliko yanayoendelea ya IPPF.
- Mipango na bajeti za ukaguzi wa ndani inaweza ‘kukadiria yasiyotarajiwa’ na kutoa posho ya ili kushughulikia shughuli za dharura.
- Wakaguzi wa ndani wanapaswa kuwasilisha matokeo ya programu ya uhakiki wa ubora kwa kamati ya fedha, jambo ambalo linaweza kuainisha mahitaji ya rasilimali kwa baraza la madiwani wakati bajeti ya mwaka ya Halmashauri inajadiliwa na kupitishwa.
- Inawezekana kutengeneza mfumo shirikishi wa kupanga, ufuatiliaji na tathmini ya programu ya maendeleo ya wafanyakazi katika ngazi ya serikali ya mitaa na serikali kuu ili kuimarisha uratibu wao na kuhakikisha kwamba ujuzi na utaalamu wa kada ya ukaguzi wa ndani unalingana na maeneo ya vihatarishi yaliyopewa kipaumbele.

Kuimarisha mchakato wa kuripoti ili kuhakikisha kuwa matokeo ya ukaguzi yanazingatiwa ipasavyo katika kazi ya uangalizi

- IAGD na mamlaka nyingine za serikali kuu zinaweza kutumia ratiba ya mawasiliano kuratibu majibu ya mapendekezo ya ukaguzi kutoka ngazi ya serikali za mitaa.
- Wakaguzi wa ndani wanapaswa kutoa taarifa kwa kamati ya fedha ya halmashauri, ambayo ina jukumu la kudhibiti na kusimamia fedha za Halmashauri.

- Wakaguzi wa ndani wanapaswa kuwa na mamlaka ya kuwasilisha ripoti ya ukaguzi wa ndani kwa kamati ya fedha ikiwa majibu ya menejimenti yanachelewa kutolewa bila sababu za msingi.
- Wakaguzi wa ndani wanatakiwa kukutana na kamati ya fedha bila uwepo wa menejimenti ili kuhakikisha mkaguzi wa ndani anafanya kazi kwa uhuru na bila upendeleo.
- Wakaguzi wa ndani wanapaswa kuwa na mwongozo unaohusu mahitaji ya kisheria ili waweze kuripoti mambo wanayoyaona au hisia za kutofuatwa kwa sheria na kanuni au udanganyifu.
- Wajumbe wa kamati ya fedha wanaweza kupokea taarifa na mafunzo zaidi ili kuelewa masuala ya ukaguzi na jinsi yanavyoathiri wajibu wao wa kudhibiti na kusimamia fedha za Halmashauri.

Kuimarisha mchakato wa ufuatiliaji ili kuhakikisha kuwa athari zinapunguzwa hadi kiwango kinachokubalika

- Ripoti za ukaguzi wa ndani zinaweza kuchanganua makadirio ya athari na mapendekezo ambayo yaliripotiwa kutekelezwa, kutekelezwa kwa kiasi, au kutotekelezwa kabisa.
- Chombo cha uangalizi cha Mamlaka ya Serikali za Mitaa kinaweza kulinganisha mapendekezo ya makadirio ya vihatarishi yaliyotekelezwa kwa kiasi au ambayo hayajatekelezwa na maelezo ya menejimenti ya kimantiki ili kutathmini kama vihatarishi hivyo vinakubalika kwa taasisi. Chombo cha cha uangalizi kinapaswa kuchukua hatua zinazofaa za kiutawala au kinidhamu dhidi ya watu binafsi au taasisi husika.
- IAGD inaweza kufanya uchambuzi wa gharama za mapendekezo ya ukaguzi.

Orodha ya Marejeo

Allen, Hemming, Potter (2013), The International Handbook on Public Financial Management.

German Corporation for International Development (2014), Accounting and Administrative Controls, Participants' Handbook.

German Corporation for International Development (2014), Functioning of Audit Committees, Participants' Handbook.

German Corporation for International Development (2014), Risk Management, Participants' Handbook.

Good Financial Governance Programme (2018), Strategy for the further development of the Internal Audit System of the Public Sector of Tanzania, Phase I: Stock Taking and Assessment and Phase II: Root Cause Analysis.

Good Financial Governance Programme (2019), Compliance Verification of Internal Audit Reports of Selected Institutions in the Tanzanian Public Sector, Mid-Term Review Report.

Institute of Internal Auditors (2009), Code of Ethics.

Institute of Internal Auditors (2012), Supplemental Guidance: The Role of Auditing in Public Sector Governance.

Institute of Internal Auditors (2012), The Three Lines of Defense in Effective Risk Management and Control.

Institute of Internal Auditors (2013), Global Internal Audit Competency Framework.

Institute of Internal Auditors (2013), Model Internal Audit Activity Charter.

Institute of Internal Auditors (2017, Internal Audit and External Audit – Distinctive Roles in Organizational Governance,), Global Perspectives and Insights, Issue 8.

Institute of Internal Auditors (2017), International Standards for the Professional Practices of Internal Auditing (Standards).

INTOSAI GOV 9140, Internal Audit Independence in the Public Sector.

INTOSAI GOV 9150, Coordination and Cooperation between SAIs and Internal Auditors in the public sector.

ISA 260 (Revised), Communicating with those charged with governance.

ISA 265, Communicating deficiencies in internal control to those charged with governance.

Ministry of Finance and Planning (2016), Five-Year Development Plan 2016/17-2020/21.

Ministry of Finance and Planning (2017), Assessment of the Public Finance Management Systems of the Central Government Applying the PEFA 2016 Framework.

Ministry of Finance and Planning (2017), Public Financial Management Reform Programme V.

Ministry of Finance and Planning and Good Financial Governance Programme (2019), Strategy for the Further Development of the Internal Audit System in the Public Sector of Tanzania.

National Audit Office (2019), Annual General Report on the Audit of the Local Government Authorities (LGAs) for the Financial Year 2017/2018.

Local Government Finance Act (1982)

Local Government Financial Memorandum (2009)

President's Office – Public Service Management and Good Governance (2022), Approved Functions and Organisation Structure of the President's Office – Regional Administration and Local Government.

Planning Commission, (no date), Tanzania Development Vision 2025.

PriceWaterhouseCoopers (2016), Consolidated Sub-National Government PEFA Assessment report.

Public Finance Act (2010)

Public Finance Regulations (2004)

Richard Brown (1968), A History of Accounting and Accountants, Psychology Press.

Sridhar Ramamoorti (2003), Chapter 1 Internal Auditing: History, Evolution, and Prospects, The Institute of Internal Auditors Research Foundation.

Sikika inafanya kazi ya kuhimiza uboreshaji wa mifumo ya afya na usimamizi wa fedha kupitia uwajibikaji jamii na uraghibishi katika ngazi zote za Serikali

Kiwanja Na. 1387C
Barabara ya Haile Selassie
Mtaa wa Mwaya, Masaki
S. L. P 12183
Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 222 600 943

Ujumbe mfupi: 0688 493 882
Nukushi: +255 22 26 680 15
Barua pepe: info@sikika.or.tz
Tovuti: www.sikika.or.tz
Twitter: @sikika1
Facebook: Sikika1
Instragram: Sikika1
LinkedIn: Sikika Tanzania

Nyumba Na. 340
Mtaa wa Kilimani,
S. L. P 1970
Dodoma, Tanzania.
Simu: 026 23 21307
Nukushi: 026 23 21316